SUPA JACKPOT
TZS. 1,114,965,687
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Rekodi** mpya yawekwa Yanga ikitinga fainali CAF

UKURASA 24




UKURASA 11


# Nipashe

Alhamisi Mei 18, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581314

www.ippmedia.com

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




# Saa 5 zilizomaliza mgomo Kariakoo

• **Wafanyabiashara** waridhia kufungua maduka...*Ukurasa 2*



Sehemu ya wafanyabiashara wakimsikiliza Waziri Mkuu, Kassimu Majaliwa (picha juu), katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### WABUNGE WASHTUKA WAHADHIRI WA VYUO KUFUNGUA BAA, SALUNI

WABUNGE wameibua hoja sita katika mjadala wa makadirio ya mapato na...



Kamishna wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima nchini (TIRA), Dk. Baghayo Saqware (wa pili kulia), akimkabidhi Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, leseni ya kuanzisha kampuni tanzu ya huduma za bima ya CRDB Insurance Company Ltd, jijini Arusha jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## CWT yazidi kukimbiwa, walimu 120 watimka

UKURASA 3



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Taifa, Freeman Mbowe (katikati), akifurahia jambo na Makamu wake, Tundu Lissu wakati wa uzinduzi wa Operesheni #255 Katiba Mpya, mjini Kigoma jana. Kulia ni Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mbowe: Tutatafuta Katiba Mpya mtaa hadi kitanda

• **Operesheni** maalum yazinduliwa Kigoma...

*Endelea ukurasa 2*

**SIASA** NDUGAI AFICHUA SIRI KUJIUZULU USPIKA UK.5

**KATUNI** UK.6



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akipiga makofi baada ya kuwasha taa kwenye nyumba ya Mama Gladness Gilole, katika Kijiji cha Sale, alipozindua mradi wa umeme vijijini (REA) katika vijiji mbalimbali vya Wilaya ya Ngorongoro, mkoani Arusha jana. **PICHA: OMR**

# Saa 5 zilizomaliza mgomo

**Na Waandishi Wetu**

KWA zaidi ya saa tano Waziri Mkuu, Kassimu Majaliwa alisimama jana kuwasikiliza wafanyabiashara wa Soko la Kariakoo jijini Dar es Salaam waliowasilisha kero zinazowakabili, hata kufikia kusitisha mgomo ulioanza Jumatatu.

Katika kikao hicho, Waziri Mkuu alitoa nafasi kwa wafanyabiashara hao, mmoja mmoja na kumalizia na viongozi wao kuongea bila hofu huku akiahidi kuwalinda dhidi ya yeyote atakayetaka kuwazuia kusema.

Wafanyabiashara hao walieleza kero 20 zinazowakabili ikiwamo kukithiri kwa rushwa, kodi mpya ya maghala ya kuhifadhia mizigo, uonevu unaofanywa na polisi, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Manispaa ya Ilala na kamatakamata inayoendeshwa na kikosi kazi.

Baada ya kuwasikiliza, Waziri Mkuu aliunda timu ya watu 14 ikijumuisha wafanyabiashara saba na viongozi saba wa serikali kwa ajili ya kukusanya maoni ya wadau kwa muda wa wiki mbili kisha kuyawasilisha kwa mawaziri.

Aliwataja wajumbe kutoka serikalini ni Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi Maalum, Katibu Tawala Mkoa wa Dar es Salaam, Mtendaji Mkuu wa Sera na Utafiti wa TRA na Kamishna Mkuu wa Kodi za Ndani.

Upande wa wafanyabiashara wajumbe wake ni Mwenyekiti wa Soko hilo la Kimataifa, Mwenyekiti wa soko hilo Kitaifa, Issa Masoud. Pia wamo Fredy Vunjabei, Omari Hussein na wengine wawili waliotajwa kwa majina ya Mpandila na Mama Bonge.

Alisema dhamira ya dhati ya Rais Samia Suluhu Hassan ni kuendeleza sekta ya kibiashara ili kila mtanzania anayeamua kufanya biashara, apate tija na maelekezo ya wasaidizi wake ni kuifanyia kazi.

Alisema ana taarifa kuwa baadhi ya maofisa wa TRA wamekuwa wakiwajibu wafanyabiashara kwamba maagizo ya Rais Samia ni ya kisiasa, hivyo wanataka barua ili kutengeneza nafasi ya kuwaonea wafanyabiashara.

"Jambo hilo si kweli. Makamu wa Rais, Rais mwenyewe na mimi Waziri Mkuu tunapotoa kauli, ni agizo kwa viongozi wote waliopo chini yetu. Wanatakiwa kutekeleza. Sasa unataka Rais aandike barua, ataandika ngapi?" alihoji.

### KUFUNGUA BIASHARA

Aliwaomba wafanyabiashara hao kufungua biashara zao akisisitiza kuwa soko hilo ni la kimataifa na nchi nyingi zinalitegemea, ombi ambalo lilipokewa na wafanyabiashara hao baada ya kuridhishwa na majibu yake.

"Lingine ni hili la askari wa Jeshi la Polisi kujihusisha na ukamataji wasiolipa kodi. Hii sio kazi yao! Tuwaache TRA wafanye kazi yao ili kuepusha mkanganyiko kama huu tena," aliagiza.

### WAFANYABIASHARA WAFUNGUKA

Wakizungumza katika viwanja vya Mnazi Mmoja jana, wafanyabiashara hao walitaja malalamiko hayo kuwa ni kulipishwa kodi ya stoo na makadirio ya kodi kubwa yasiyoendana na bidhaa zilizopo.

Pia walitaja kuongezeka kwa machinga wasiostahili na polisi wa barabarani kukamata mizigo na kuleta usumbufu usio na tija, hali inayochochea kuwapo rushwa.

Vilevile, waliiomba serikali kufumua mfumo wa ulipaji kodi wa TRA kwa madai kuwa hauendani na hali halisi za biashara zao, hivyo kuwarudisha nyuma kimaendeleo.

Mfanyabiashara Elimringi Goodluck alisema sababu kubwa wafanyabiashara hao kufunga maduka yao ni kodi mpya ya stoo. Alimtaka Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, kuipeleka sheria hiyo bungeni kwa hati ya dharura, ili kuifuta au kuiboresha na kuwapo na kodi rafiki ambazo kila mfanyabiashara atazimudu.

Mfanyabiashara Daudi Maginge, alilalamikia kuwapo wafanyabiashara raia wa China katika soko hilo wanaouza bidhaa kwa bei ya rejareja sawa na wazawa badala ya kuwekeza katika viwanda. Alisema wanaua biashara zao.

Pia alisema ujenzi wa soko kubwa la kuuza la bidhaa za China kwa bei ya jumla Afrika Mashariki huko Ubungo mkoani Dar es Salaam kutaua Soko la Kariakoo kwa kuwa wafanyabiashara waliokuwa wananunua katika maduka hayo, watahamia katika gulio hilo kupata bidhaa kwa bei nafuu.

Mfanyabiashara wa vifaa vya magari, Awadh Mpalila, aliiomba serikali kufumua mfumo wa kodi ya forodha bandarini kwa kuwa sio rafiki kwa wafanyabiashara wanaoagiza bidhaa zao nje ya nchi.

### MAWAZIRI WABEBESHWA LAWAMA

Mwenyekiti wa Wamiliki wa Malori Wadogo na Wa Kati, Chuki Shabani alimtupia lawama Waziri wa Fedha, Dk. Nchemba, kwa kuongeza kodi kubwa isiyolipika kwa wasafirishaji kutoka Sh. 800,000 hadi milioni 2.79.

"Sasa kwa kuwa Waziri Mkuu unatulinda, ninasema hivi... hiki kiburi cha TRA kinasababishwa na bosi wao (Waziri Fedha), ndio maana kuna kodi lukuki, hakuna pa kukimbilia," alisema.

Pia alisema kauli ya Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, kuwa waliofunga maduka Kariakoo ni kwa hiari yao, ni ya kudharau na kupuuzia matatizo wanayokabiliana nayo wafanyabiashara hao, hivyo hastahili kuwa katika hiyo nafasi.

Mwenyekiti wa Jumuia ya Wakala wa Forodha Zanzibar, Hussein Omari, alisema bandari watoze kodi ya 'storage' stahiki kwa wafanyabiashara wa Zanzibar kwa kuwa mizigo inayotoka Zanzibar inaanza kutozwa gharama mara tu inapofika bandarini wakati inayotoka Dubai inaanza kutozwa kodi baada ya siku saba.

Mwenyekiti wa Wafanyabiashara wa Kanda ya Juu Kusini, Sifaeli Msigala, alimwomba Waziri Mkuu kuunda kamati itakayojadiliana na TRA namna ya kufanya, ili kuweka kodi rafiki kwa wafanyabiashara hao.

Mwenyekiti wa Wafanyabiashara wa Soko la Kariakoo, Martin Mbwana, alimwomba Waziri Mkuu kumwagiza Kamishna wa TRA, Alphayo Kidata, kuwaondoa maofisa wa TRA, maarufu vishoka na polisi waliotajwa ili kulinda usalama wa wafanyabiashara waliowataja kwa sababu wanaweza kuwashughulikia.

***Imeandikwa na Jenifer Gilla na Halfani Chusi***

## Mbowe: Tutatafuta katiba mpya mtaa hadi kitanda

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo(CHADEMA), kimezindua operesheni maalum iliyopewa jina la #255 Katiba Mpya, itakayoanza hivi karibuni kwa kufanya mikutano nchi nzima.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa operesheni hiyo iliyofanyika mkoani Kigoma jana, Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe, alisema wamepanga kuzunguka nchi nzima bila kupumzika mpaka Uchaguzi Mkuu ujao.

Alisema baada ya uzinduzi huo, watapita nchi nzima, kitongoji kwa kitongoji, kijiji kwa kijiji, mtaa kwa mtaa, kitanda hadi kitanda na kata kwa kata kudai mchakato wa katiba mpya.

Alisema katika kufanikisha operesheni hiyo, wamegawanya mikoa yote katika kanda nane ambazo watapita kwa kutumia anga, barabara na hata kwa njia ya maji.

Alisema lengo ni kutaka katiba mpya ili kubadilisha mfumo ambao viongozi wote wanaopatikana katika uchaguzi unaokuja wawe ni wa kuchaguliwa na wananchi pekee.

Mbowe alisema katiba mpya itakuwa suluhisho katika kupunguza madaraka makubwa aliyopewa Rais katika kuamua hatma ya watanzania.

"Tunakwenda kuandaa chama, kuandaa wenyeviti wa mitaa, vijiji na vitongoji ili tuwe na sauti. Tutapigana vita hii ya katiba kwa njia ya anga, magari, baiskeli na hata mitumbwi. Tunataka uchaguzi ujao sisi tusiwe wa kulia kuibiwa kura tena. Na tunataka tujenge mtandao kuanzia kule chini ndipo tukipandishe. Tulipotoka kwenye miaka saba ya bonde la uvuli wa mauti tuliumizwa sana.

"Tulipopitia wakati ule tulilazimika kutumia mbinu zote na wakati mwingine tulilazimika kubadili gia angani. Lazima turekebishe nchi hii na msingi wa kurekebisha lazima ujikite kwenye katiba.

"Hatuwezi kusema hakuna tulichokifanya kwenye vikao vya maridhiano, hata mikutano hii tunayofanya ni matokeo yake japokuwa ni haki yetu kikatiba kufanya mikutano hii. Mazungumzo yetu yamesaidia wengi, wafungwa wa kisiasa kutolewa isipokuwa wawili waliobaki, tumewarejesha kwenye mchakato wa katiba mpya kwa sababu wao hawakuwa na haraka.

"Leo tunaona wafanyabiashara wa Kariakoo wanaweza kugoma na sisi tunawaunga mkono na wameumizwa kwa miaka mingi, lakini kupata nguvu ya kufanya hivyo kwa sasa ni hatua kubwa. Tutaendelea na mazungumzo lakini lazima tupambane kwenye kila njia nyingine inayowezekana, na tunasema katiba mpya ni sasa na tunapaswa kuisimamia wakati wote," alisema.

### UHUSIANO WAKE NA LISSU

Mbowe pia alisema amesikia kauli kwamba hakuna maelewano kati yake na Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Tundu Lissu na kuweka wazi kwamba hakuna kitu kama hicho.

"Nimesikia watu wanasema '...ooh Mbowe na Makamu wake hawaelewani... hatuelewani?" Mbowe alihoji.

Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika, alisema ili mckakato wa katiba mpya uanze, ni lazima sheria ipelekwe bungeni, kutengwe bajeti kwa ajili ya kuendeleza mchakato huo na wamebaini fedha zilizotengwa hazitoshi kukamilisha mchakato huo.

"Tunataka hilo Bunge linaloendelea litenge fedha ya kukamilisha mchakato huo na tunataka hilo liwe ni azimio letu. Badala ya matumizi mengine ya anasa kama ilivyoainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG), tunataka fedha zitengwe kwa ajili ya masuala muhimu kama ya mchakato wa katiba mpya," alisema.

Naibu Katibu Mkuu wa CHADEMA Zanzibar, Salum Mwalimu, alisema kuna haja kuufumua muundo wa sasa wa Muungano na kuunda wa serikali tatu na kuomba watanzania wa pande zote mbili za Muungano huo kupewa nafasi ya kuujadili na kutoa maoni yao namna wanavyotaka uwe.

Lissu alisema katiba bora huwa inaanzia kwa uraia. Katiba ya sasa haisemi chochote juu ya uraia wa mtanzania yeyote. Wanahitaji katiba mpya itatue tatizo la uraia ili usihojiwe tena.

"Suala la katiba mpya linahusu Watanzania wote waliopo nchini na wale ambao wametengeneza familia nje ya nchi. Uraia wetu utokane na damu yetu hata kama mtu atabadilisha magamba," alisema Lissu na kusisitiza wanataka katiba mpya na Tume huru ya Uchaguzi kabla ya uchaguzi mkuu ujao.

## HABARI KITAIFA

# Zaidi walimu 200 wajiondoa CWT

**Na Vitus Audax,** MWANZA

ZAIDI ya walimu 200 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti, mkoani Mara wamewasilisha katika ofisi ya Ofisa Utumishi Wilaya, barua za maombi ya kujiondoa katika Chama cha Walimu Tanzania (CWT) huku wengine 120 wakijiondoa katika chama hicho na kujiunga na Chama cha Kulinda na Kutetea Haki za Walimu Tanzania (CHAKUHAWATA).

Hata hivyo, Katibu wa CWT Wilaya ya Serengeti, Clophode Mkwama, alisema, chama hicho hakijapokea notisi ya mtu yeyote kati ya hao 200 wanaohitaji kujiondoa.

Peter Kaboyoka, miongoni mwa walimu 120 waliojiondoa CWT kutoka Shule ya Sekondari Mugumu akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu jana, alisema ana zaidi ya miezi tisa tangu ajiunge na CHAKUHAWATA kisheria na kwa sasa hakatwi makato ya asilimia mbili kutoka CWT.

Alisema sababu ya kujiondoa katika chama hicho ni kutoridhishwa na utaratibu wa kutotoa taarifa za mapato na matumizi sambamba na makato makubwa ya asilimia mbili ambayo yanaongezeka kila uchwao.

"Nilikuwa nikikatwa Sh. 19,000 kila mwezi na hii ni tofauti kwa kila mwalimu kutokana na kiwango chake cha mshahara hivyo mshahara ukiongezeka tu na makato yanaongezeka utaratibu unaotuumiza kama walimu huku tukishindwa kujua faida ya wingi wa makato hayo huku katika chama kipya anakatwa Sh. 5,000 ambayo haiongezeki kwa asilimia," alisema Kaboyoka.

Kuhusu utaratibu wa kujiondoa, alisema walifuata taratibu zote ikiwa ni pamoja na kujaza fomu ya kujiondoa CWT licha ya kukumbana na changamoto kwa zaidi ya miezi minne, lakini alifanikiwa kujiondoa na sasa katika malipo yake analipwa Sh. 5,000 ya CHAKUHAWATA.

Katibu wa CHAKUHAWATA Wilaya ya Serengeti, Samson Mgutu, aliiambia Nipashe kuwa mpaka sasa wamepokea wanachama 120 na tayari wanapata stahiki zao kwa mujibu wa sheria licha zaidi ya wanachama 200 maombi yao kukwama katika ofisi ya Utumishi wa Umma wilaya.

Aidha, alisema walimu hao wamefuata utaratibu wote wa kujaza fomu tatu ikiwamo ya kuomba kuwa mwanachama wa chama kipya na kuhama chama cha zamani, kupitisha makato ya CWT ya asilimia mbili pamoja na fomu ya TUF 16.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, Katibu Mkuu CWT, Japheth Maganga, alisema suala la kuhama kwa walimu kitaifa hawezi kulijibia.

Kuhusu taarifa za wanachama kujiondoa katika chama hicho, Katibu wa CWT Wilaya ya Serengeti, Clophode Mkwama, alisema, chama hicho hakijapokea notisi ya mtu yeyote kati ya hao 200 wanaohitaji kujiondoa katika chama hicho licha ya kupokea barua kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ikihitaji ufafanuzi kuhusu wanachama wanaoendelea kujiondoa katika chama hicho.

Aidha, alisema chama hicho tayari kimemwandikia barua Mkurugenzi wa halmashauri hiyo kujua vigezo na utaratibu uliotumika kuidhinisha kuondoka kwa wanachama 120.



Mkurugenzi wa Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni, Seleman Bishagazi (kulia), akitoa elimu kuhusu madhara ya rushwa ya ngono kwa viongozi wa vikundi mbalimbali vya kijamii, katika Kata ya Buza, mkoani Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wabunge washtuka wahadhiri wa vyuo vikuu kufungua baa na saluni

**Na Romana Mallya,** DODOMA

WABUNGE wameibua hoja sita katika mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2023/24.

Hoja hizo ni miundombinu hatarishi shuleni na vyuoni, mwonekano mbaya wa vijana walioko vyuoni, kuongezeka kwa wanafunzi wanaoondolewa chuoni baada ya kufeli mitihani, maslahi duni ya wahadhiri wa vyuo ambapo baadhi yao wamelazimika kufungua saluni na baa, idadi ndogo ya walimu na shule aliyosoma Rais kutokuwa na maktaba.

Katika mjadala huo ulioanza juzi, Mbunge wa Vwawa, Japhet Hasunga (CCM), alisema kuwa bila maarifa na ujuzi, umaskini hauwezi kupungua na kuondokana na athari za kiuchumi.

Alisema mabadiliko ya mitaala yataacha alama ndani ya nchi kwa kuwa elimu inatakiwa kuendana na ajenda ya nchi. Hasunga aliongeza: "Tunataka kuona mageuzi ya ufundishaji uendane na mitaala tunayohitaji, lazima tuwe na vifaa vya kuwaandaa vijana."

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Dk. Thea Ntara, alisema mikoa ya Mtwara na Ruvuma haina vyuo na hata vile vya sekta binafsi vingi vimekufa na kuomba wasaidiwe.

"Hatuna miradi mikubwa. Wakati mnafikiria kujenga chuo cha IT Dodoma niliwaza sana. Kwanini hamkukipeleka Ruvuma? Dodoma ina UDOM (Chuo Kikuu cha Dodoma) na kimekuwa kikubwa na kina changamoto za kutosha.

"Kila siku mnaongea hapa kuwa UDOM ni kikubwa Afrika Mashariki. Mheshimiwa Naibu Spika, nenda pale utashangaa, yaani majengo yanaporomoka. Dari inaanza kudondoka, vigae chini vimepasuka, mabomba ya maji yamepasuka, halafu nimekwenda pale nikaingia katika choo, yaani mpaka unaona aibu.

"Kuna mlipuko utatokea. Maji yanapotea pale kwa sababu mabomba yote yamepasuka na wana upungufu wa maji karibu lita milioni 1.1. Serikali mpo, sitaki Mheshimiwa Waziri tuongozane, nenda ukaone UDOM. Hali ni mbaya," alisema.

Pia alisema zipo shule kongwe ikiwamo aliyosoma Rais wa Awamu ya Tatu, Hayati Benjamin Mkapa, haina maktaba na ina kidato cha tano.

Mbunge wa Hai (CCM), Saashisha Mafuwe, aliitaka serikali kuboresha maslahi ya wahadhiri wa vyuo vikuu na kuongeza idadi yao, akionya kuwa wasipotazama eneo hilo na kuwapa heshima stahiki, hata mitaala wanayokwenda kuiandaa haitosaidia kwa sababu watekelezaji na wasimamizi ni hao.

"Unakuta mwalimu anayesimamia utafiti ana wanafunzi zaidi ya 20, hebu niambie tunakwenda kutengeneza watu wa PhD (Shahada ya Uzamivu) wa aina gani? Mimi ni mwanafunzi wa PhD UDOM, ninaona ugumu ulivyo, unamtafuta mwalimu wiki tatu.

"Na si kwa makusudi anafanya hivyo, ana wanafunzi wengi. Akitoka hapo unakuta anamiliki saluni Dodoma. Hata waliko kule SUA (Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo) ambao tungetegemea wamiliki mashamba, wamiliki mifugo, unakutana nao wanamiliki baa huko. Kwanini wanafanya hivyo? Stahiki zao hazitoshelezi.

Akizungumzia nidhamu za wanafunzi vyuo vikuu, mbunge huyo alisema endapo hawatolitazama, litaleta shida kwa kuwa wengi wanasoma shahada kwa lengo la kuandaliwa kuwa viongozi.

"Ukipita Dodoma unajifunza jambo gani au pale UDOM ukimwona kijana wa mwaka wa tatu? Je, anafanana kuandaliwa kuwa kiongozi na msimamizi wa taasisi za serikali? Wakati mwingine wahadhiri kule wanalalamika eti sisi wanasiasa wakiguswa kidogo sisi ndio tunawatetea, hawa ndio viongozi tunaowaandaa? Ukimwona leo mtoto wa shahada huwezi kumtofautisha aliyeko kidato cha pili na wa shahada.

"Utakutana na mtoto kavaa ndala, unakutana naye kwenye mitaa, mwonekano wa kuandaliwa kuwa kiongozi haupo. Wenzetu SAUT (Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino) wamejitahidi, mambo ya nidhamu yanakwenda sambamba na utoaji wa taaluma," alisema.

Mbunge wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara, alisema kuna upungufu mkubwa wa mahitaji ya elimu kwa walimu wenyewe, akifafanua: "Kiingereza anafundisha anakijua? Kiswahili hicho anakijua? Kifaransa anakijua? Au ni walimu wanaofundisha Kiswahili shuleni?"


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
17.05.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **19.05.2023** hadi **25.05.2023** kampuni ya **CEVA Interfreight** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Bandari ya Dar Es Salaam** kuelekea **Mzenga,** gari hilo lenye namba za usajili **NRB97300 / NRB15200**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - Mita 29.5**
   **Upana - Mita 5.50**
   **Kimo - Mita 4.80**

3. Njia itakayotumika: **Banadari ya Dar Es Salaam hadi Mzenga station kupitia Morogoro road na Mlandizi,** gari litasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

# CRDB yapewa leseni kuanzisha kampuni tanzu ya bima nchini

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

KATIKA kutanua huduma za bima nchini, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) imeipa Benki ya CRDB leseni kuanzisha kampuni tanzu ya bima ijulikanayo kama CRDB Insurance Company (CIC) Ltd, hivyo kuwa benki ya kwanza nchini kumiliki kampuni kamili ya bima.

Akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi leseni hiyo iliyofanyika katika Hoteli ya Gran Melia jijini Arusha jana, Kamishna wa Bima, Dk. Baghayo Saqware, aliipongeza Benki ya CRDB kwa kukua katika utoaji wa huduma za bima kutoka kuwa wakala mpaka kampuni kamili ya bima.

"CRDB Insurance ni mtoto mpya kwenye soko la bima na mtoto mwingine kwa Benki ya CRDB katika soko la fedha nchini. Inafurahisha kuona mnakua kutoka hatua moja kwenda nyingine. Ninaamini ndani ya miaka mitano ijayo mtakwenda kwenye hatua nyingine kubwa zaidi ya hii. Kuna fursa kubwa kwenu kukua katika soko letu," alisema Dk. Saqware.

Kamishna Saqware alisema kwa uzoefu ambao Benki ya CRDB inao katika sekta ya bima, TIRA ina imani CRDB Insurance Company (CIC) Ltd itakwenda kusaidia utekelezaji wa lengo la serikali la kuchochea ujumuishi wa wananchi katika huduma za bima ili Watanzania wanaotumia bidhaa zake wawe walau asilimia 50 ifikapo mwaka 2030 kutoka asilimia 18 ya sasa.

"Katika kuchochea ujumuishi wa kibima, serikali imepitisha sheria ya kufanya baadhi ya bima kuwa za lazima ikiwamo bima ya majengo, makandarasi, afya na za vyombo vya usafiri. Mkiweza kuja na mkakati madhubuti wa kuchangamkia vizuri maeneo haya na kuhudumia kwa walau asilimia 30, niwahakikishie ndani ya kipindi kifupi mtatoka kuwa kampuni changa na kuwa moja ya kampuni kubwa za bima nchini," alisema Dk. Saqware.

Akipokea leseni hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema ni furaha kubwa kwao kupata leseni ya huduma za bima za jumla (general insurance) ukiwa ni muda mfupi tangu walipopata leseni ya kutoa huduma za benki Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

"Benki ya CRDB inayo historia kubwa ya kufanya biashara ya bima kwa kuwa takriban miaka 15 iliyopita imekuwa inaifanya kwa namna tofauti ikianza kama wakala na sasa ni kampuni kamili ya bima. Mafanikio haya yanadhihirisha mazingira rafiki ya kufanya biashara nchini," alisema Nsekela.

Alisema CRDB Insurance Company itajikita katika ubunifu wa bidhaa na huduma za bima za jumla kwa kuzingatia viwango vilivyo bora na kuhakikisha huduma hizo zinawafikia wananchi walio wengi ili kuchochea maendeleo ya uchumi wa nchi.

"Malengo yetu ni kuwa kiongozi katika sekta ya bima nchini kama ilivyo kwa benki yetu na kampuni zetu tanzu zingine. Lakini ili kuwa kiongozi ni lazima tuweze kutoa huduma zilizo bora na za mfano katika soko, lazima tuweze kuwekeza katika miundombinu ya usambazaji na uuzaji wa bima ikiwamo kuwatumia mawakala, madalali, Banc Assurance na majukwaa ya kidijiti kuuza bima. Ninaomba nikuhakikishie Kamishna tumejipanga kutekeleza hayo yote," alisema Nsekela.

Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Insurance Company Ltd, Wilson Mnzava, alisema wamejipanga kikamilifu kuanza kutoa huduma za bima kwa wananchi kuanzia bima zote za jumla huku akieleza kuwa tayari kampuni hiyo imeshaanza mchakato wa kuleta huduma zenye ubunifu za bima katika sekta za kimkakati nchini ikiwamo sekta ya kilimo.

"Ninapenda kuwakaribisha Watanzania wote binafsi, taasisi na kampuni kupata huduma katika Kampuni yao ya CRDB Insurance Company Ltd. Niwahakikishie wananchi kwamba CRDB Insurance Company Ltd ndio chaguo sahihi kwao. Tumejiandaa kikamilifu kuwahudumia. Nikuahidi Kamishna kuwa kampuni yetu itashirikiana kwa karibu na TIRA kuboresha huduma na kuyafikia matarajio ya sekta ya bima kwa ujumla," alisema Mnzava.

Taarifa za TIRA zinaonyesha mpaka Desemba 2022, kulikuwa na kampuni 32 za bima nchini, hivyo CRDB Insurance Compaany Ltd inakuwa kampuni ya 33. Katika kipindi hicho, pia kulikuwa na mawakala wa bima 1,500, benki 32 zinazotoa huduma za bima na kampuni tano zinazotoa huduma za bima kidijitali.

Kwa sasa sekta ndogo ya bima inachangia asilimia 1.68 kwenye pato la taifa, malengo yaliyopo ni kufikisha asilimia tatu hadi mwaka 2030 na dalili za kufanikisha hilo zinaonekana kwa kuwa mwaka 2022 tozo za bima zilizolipwa (premiums) zilikuwa na thamani ya Sh. trilioni 1.154 kutoka Sh. bilioni 913 mwaka 2021.




Katibu Tawala Msaidizi Mkoa wa Arusha, David Francis Lyamongi (wa pili kushoto), akikabidhi kitendea kazi kwa Japhet Mollel mmoja wa vijana waliohitimu mafunzo ya VETA kupitia mradi wa KCB 2jiajiri jijini Arusha juzi. Mradi huo wenye thamani ya Sh. bilioni 2.2 umefadhiliwa na KCB Foundation pamoja na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) na kuwanufaisha vijana 960 nchini. Kushoto ni Mkuu wa Masoko, Mawasiliano na Uhusiano wa Benki ya KCB, Christine Manyenye na (kulia) ni Kaimu Msajili wa VETA Arusha, Abraham Mbuguni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

KELELE IBADANI

## Jumuiya ya Amani na NEMC wateta

**Na Mwandishi Wetu**

JUMUIYA ya Maridhiano na Amani Tanzania imekutana na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kuzungumzia kelele katika nyumba za ibada.

Hatua hiyo ni utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa la kukutana na jumuiya hiyo, ili kujadili na kuweka sawa masuala ya kelele katika nyumba za ibada.

Akizungumza jana, Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Shekhe Alhad Mussa, alisema Waziri Mkuu alikabidhi jambo hilo kwa jumuiya hiyo, ili kushirikiana na serikali kupitia NEMC na kufikia mwafaka.

"Sisi tumepokea kauli ya Waziri Mkuu na tumeanza kufanyia kazi. Leo (jana) tumekutana na NEMC viongozi wakuu wa jumuiya, ili kupeleka elimu hiyo kwa wenzetu. Hatimaye tukitoka tuwe na makubaliano ya pamoja ambayo hayataumiza mtu," alisema.

Alipongeza NEMC kwa elimu waliyoitoa na kwa usimamizi mzuri wa sheria ya mazingira na kutoa elimu kwa makundi mbalimbali.

"Wamejitahidi kutoa elimu kwa makundi mbalimbali juu ya kudhibiti kelele. Tunashukuru sana NEMC kupitia Mkurugenzi Mkuu kwa kazi nzuri wanayofanya, lakini pia na kuchukua hatua tumeona NEMC imeanza kuchukua hatua, lazima tupongeze hatua hizi maana mara nyingi huwa tuna sheria katika maandishi lakini utekelezaji haupo," alisema.

Kadhalika, alisema NEMC imeonyesha mfano mzuri kwa kuchukua hatua kutokana na wananchi kulalamika sana kuhusu kelele.

"Tumeelewa madhara ya kelele na sisi viongozi wa dini tutahakikisha tunaisaidia serikali kupitia NEMC, ili watu wetu wapate elimu ya kutosha na kuona madhara haya yanaondoshwa kwa pamoja kwa wananchi," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema baraza linaheshimu kazi ya viongozi wa dini.

# Vitambulisho vya Taifa kutumika bila ya ukomo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetoa rukhsa kwa vitambulisho vya taifa ambavyo vimefikia ukomo, viendelee kutumika na vitambulisho vijavyo havitokuwa na tarehe ya ukomo.

Hatua hiyo imetokana na marekebisho ya Kanuni za Usajili na Utambuzi wa Watu za Mwaka, 2014 ikiwamo Kanuni ya 7(3)(a) ambayo imeainisha taarifa zilizopo katika uso wa Kitambulisho cha Taifa zinazohusisha tarehe ya ukomo wa muda wa matumizi ya Kitambulisho cha Taifa ili kuondoa ukomo wa matumizi.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira, Hamza Khamis Chilo, aliyasema hayo jana bungeni alipojibu maswali ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Katika maswali hayo, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Janejelly Ntate, alihoji mpango wa serikali kuleta uelewa kwa wananchi ili wajue kwamba vitambulisho vyao ambavyo vimekaribia kufika ukomo havitowaathiri ili kupunguza taharuki kwa wananchi.

Mbunge wa Temeke (CCM), Dorothy Kilave, alitaka tamko la serikali kuhusu Kitambulisho cha Taifa kuwekwa ukomo wa kutumika.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri Chilo alisema marekebisho hayo yalitangazwa rasmi katika Tangazo la Serikali (GN) Na. 96 la Februari 17, 2023.

"Hii ina maana kwamba, Vitambulisho vya Taifa kwa raia ili kuwezesha vitambulisho vinavyofikia ukomo wake baada ya kipindi cha miaka 10 vitaendelea kutumika baada ya muda huo," alisema.

Aliongeza kuwa Namba za Utambulisho (NIN) zilizopo katika vitambulisho hivyo, hazina ukomo wa muda wa matumizi.

"Marekebisho hayo hayatahusu muda wa matumizi ya vitambulisho vya taifa kwa wageni wakazi na wakimbizi," alisema.

Alitoa wito kwa watoa huduma wanaotumia Vitambulisho vya Taifa kuwatambua wateja wao, kuendelea kutambua vitambulisho vyenye tarehe za ukomo.

Pia alisema vitambulisho ambavyo vitakuja baada ya tangazo hilo havitokuwa na ukomo, lakini hata vile vitambulisho ambavyo tangazo lilishatoka wataendelea kwa kuwa lengo la serikali ni kuhakikisha wananchi hawakosi huduma.

"Vitambulisho ambavyo vitakuja baada ya tangazo hili havitokuwa na ukomo ila kwa vitambulisho ambavyo vimekwisha muda navyo vitaendelea kutumika kuwapatia huduma mpaka pale serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani itakapotoa maelekezo mengine," alifafanua.

# Ndugai atoboa siri ya kujiuzulu

**Na Zanura Mollel**

SPIKA mstaafu, Job Ndugai, jana amefichua siri aliyoiweka muda mrefu ya kuchukua hatua ya kujiuzulu wadhifa wake wa u-Spika, mwaka jana.

Alifichua siri hiyo katika maziko ya mtoto wa Waziri Mkuu mstaafu, William Malecela, maarufu 'Le Mutuz', yaliyofanyika Mvumi, jijini Dodoma.

Alisema Januari mwaka 2022, Waziri Mkuu mstaafu, Mzee Samwel Malecela, alimfuata nyumbani kwake na kumshauri ajiuzulu katika nafasi yake na alisikia ushauri huo.

Ndugai alisema alimshauri kama kaka yake na kuamua kuchukua uamuzi huo kutokana na uzito alionao mzee Malecela katika jamii.

Ndugai aliandika barua ya kujiuzulu nafasi hiyo Januari 2022, ikiwa ni siku chache baada ya kukosoa mikopo inayochukuliwa na serikali. Katika maziko hayo, mwanasiasa mkongwe Abdallah Bulembo, alisema alifahamiana na Le Mutuz walipokutana akiwa kwenye Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) na walifanya ziara za kichama maeneo mbalimbali.

Alisema alitumia mtandao wake kukitangaza chama, kuongeza wanachama na kwamba kutokana na kazi yake Rais Jakaya Kikwete alimpigia simu na kumuuliza: "Hivi William mnamlipa kweli? Nikamjibu ndiyo, akasema mlipeni vizuri sababu anafanya kazi kubwa kuliko ninyi."

"Nachotaka kusema ni hivi, vijana mnaokua acheni kupandisha mabega, hujui kesho yako, tumepoteza mtu muhimu ambaye alikua habagui mkubwa wala mdogo," alisema Bulembo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, akitoa salamu kwa niaba ya serikali, alisema Malecela ni kiongozi mstaafu wa serikali na alishika nafasi mbalimbali ikiwamo Makamu wa Rais na Waziri Mkuu mstaafu na kwamba salamu za pole zimetoka kwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa anatambua mchango wake serikalini.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akitoa salamu za pole kwa niaba ya wabunge, alisema kifo ni jambo linaloleta mshtuko ndani ya jamii na kwamba kila mmoja anatamani kuishi na ndugu yake kwa kuwa bado anamuhitaji.

"Kifo kinatia hofu na anakiogopa na maombi yake kwa Mungu safari yake ya kifo ichelewe, tuombe Mungu atupe watu wakusimulia mema yetu, Le Mutuz nilimfahamu kama mtu mwema sijui wewe ulimfahamuje," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya CCM, Naibu Katibu Mkuu, Anaringi Macha, alisema chama hicho kimepokea kwa masikitiko taarifa ya kuondoka kwa Le Mutuz na kwamba pengo la kuondoka kwake sio la familia pekee, serikali pia imeondokewa na mwananchi mshirika wa kustawisha maendeleo ya taifa.


**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**TANZANIA ELECTRIC SUPPLY COMPANY LIMITED**

TANESCO

## Specific Procurement Notice

## Invitation for Bids (IFB)

## Procurement of EPC Contractor for Extension of 400/220kV Nyakanazi Substation and Construction of New 400/132/33kV Kigoma (Kidahwe) Substation

**CB No.:** PA/001/2021-2022/HQ/W/04
**Project:** Construction of Substations for Kigoma - Nyakanazi Transmission Line Project
**Employer:** Tanzania Electric Supply Company Limited (TANESCO)

## Invitation for Bids (IFB)

**Employer:** Tanzania Electric Supply Company Limited (TANESCO)
**Project:** Construction of Substations for Kigoma - Nyakanazi Transmission Line Project
**Contract Title:** Design, Supply, Installation, Testing and Commissioning of New 400/132/33kV Kigoma (Kidahwe) Substation and Extension of
**400/220kV** Nyakanazi Substation
**Country:** Tanzania
Loan Agreement No. and Title: TZA -13 - Construction of Substations for Kigoma-Nyakanazi Transmission Line Project
**IFB No.:** PA/001/2021-2022/HQ/W/04
**Issued on:** 18th May 2023

1. The Government of Tanzania (hereinafter referred to as the "Borrower") has received a loan through the Export-Import Bank of Korea (hereinafter referred to as the "Bank") from the resources of the Economic Development Cooperation Fund (hereinafter referred to as the "EDCF") of the Republic of Korea in an amount of Korean loan equivalent to USD 45 million towards the cost of Construction of Substations for Kigoma - Nyakanazi Transmission Line Project (herein after referred to as the "Project"), and intends to apply a portion of the proceeds of this loan to payments under the contract for which this invitation to bid is issued.

2. The Project Executing Agency now invites sealed bids from eligible bidders for Tender No. PA/001/2021-2022/HQ/W/04 on Procurement of Design, Supply, Installation, Testing and Commissioning of New 400/132/33kV Kigoma (Kidahwe) Substation and Extension of 400/220kV Nyakanazi Substation.

3. Bidding will be conducted through Competitive Bidding (CB) procedures specified in the Guideline for Procurement under EDCF Loan, and is open to all eligible bidders that meet the following minimum qualification criteria. The bidder shall be limited to those firms who are entitled eligible by the Article 4.2 through 4.5 of the Instruction to Bidders in Section of the SBD subject to the restrictions specified in Section V (Eligible Countries) which states that "a Bidder, and all parties constituting the Bidder, shall have the nationality of republic of Korea or juridical person incorporated and registered therein", and the Section of the SBD provides the qualification criteria of the Bidders.

4. Interested eligible Bidders may obtain further information from Tanzania Electric Supply Company Limited (TANESCO) and inspect the bidding documents at the address below from 09:00 to 17:00 o'clock.

5. A complete set of bidding documents may be purchased by any interested Bidders on the submission of a written application and proof of payment of the application fee to the address given below under paragraph 10 and upon payment of a nonrefundable fee of USD 200 (Two hundred US dollars). The method of payment will be direct deposit to the following account.

| | Currency | Bank | Account | SWIFT Code |
|---|---|---|---|---|
| 1 | EURO | CRDB Bank | 19J1043011100 | CORUTZ |
| 2 | USD | CRDB Bank | 02J1043011100 | CORUTZ |
| 3 | USD | CITI Bank | 0100235021 | CITITZTZ |

6. Eligible interested Bidders present in Tanzania may buy Bidding Documents at TANESCO premises and pay locally through National Microfinance Bank (NMB) upon receipt of reference number from TANESCO.

7. The document will be provided to the Bidders who paid for the tender in a soft copy.

8. This Invitation shall take effect until 21st July 2023, after publication in the official website or in a newspaper of International and general nationwide circulation.

9. Bids must be delivered to the address below at or before 21st July 2023. All bids must be accompanied by a bid security of USD 1,500,000 (One Million Five Hundred Thousand US Dollars) fixed mount. Late bids shall be rejected.

   Bids will be opened in the presence of the Bidder's representatives who choose to attend at the address below on 21st July 2023 at 10:00 AM local time.

10. The Tanzania Electric Supply Company Limited (TANESCO) will not be responsible for any costs or expenses incurred by Bidders in connection with the preparation or delivery of Bids.

**The Secretary, Tender Board,**
**Tanzania Electric Supply Company Limited,**
**Street Address: Morogoro Road, Ubungo Area,**
**Building/Plot No: Umeme Park Building,**
**3rd Floor/Room No. A 305,**
**P.O. Box 9024**
**City/Town: Dar es Salaam.**
**Country: Tanzania**
**Telephone: +255 222 210264; 210267,**
**Emails: sec.tenderboard@tanesco.co.tz**
**CC; pmuprojects@tanesco.co.tz**
**Web site: www.tanesco.co.tz**

**MANAGING DIRECTOR**
**TANZANIA ELECTRIC SUPPLY COMPANY LIMITED**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tahadhari ichukuliwe ugonjwa shinikizo la damu

**TAARIFA** ya Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, jana kuhusu ugonjwa wa shinikizo la damu imeshtua na hatua za haraka zinahitajika ili kunusuru wananchi na ugonjwa huo.

Akitoa taarifa hiyo amesema watu watatu hadi wanne kati ya 10 wana shinikizo la juu la damu katika mikoa saba ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Takwimu hizi zinaogopesha ikizingatiwa kuwa ugonjwa huu uko katika makundi ya magonjwa yasiyoambukiza ambao unaweza kudhibitiwa kwa kufuata kanuni za afya.

Mikoa iliyotajwa baada ya kufanyiwa uchunguzi wa jamii ni Pwani, Arusha, Geita, Mtwara, Lindi, Iringa na Dar es Salaam na Zanzibar.

Aidha, wagonjwa sita kati ya 10 wanaoonwa kwenye Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), wanaelezwa kuwa na ugonjwa huo.

Katika taarifa yake Waziri Ummy alibainisha hayo wakati akitoa tamko kwenye maadhimisho ya Siku ya Shinikizo la Juu la Damu Duniani yaliyoambatana na kaulimbiu isemayo 'Pima shinikizo la damu kwa usahihi, idhibiti, ishi kwa muda mrefu'.

Wagonjwa waliotibiwa JKCI tangu ilipoanzishwa Septemba 2015 hadi Aprili 2023, kati ya 619,102 waliotibiwa asilimia 66 walikuwa na tatizo la ugonjwa huo.

Ugonjwa wa shinikizo la damu pia unasababisha kiharusi, shambulio la moyo, moyo kushindwa kufanya kazi, kutuna kwa kuta za mishipa ya damu, moyo, uharibifu kwenye chujio za figo, ganzi miguuni na mikononi, upofu na kupunguza nguvu za kiume.

Serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, inaendelea na utekelezaji wa Sera ya Afya ya mwaka 2007, ambayo inalenga kutoa huduma kwa magonjwa yasiyoambukiza ikiwamo ugonjwa wa shinikizo la juu la damu kwa umahiri zaidi.

Huduma za matibabu ya shinikizo la juu la damu zimekuwa zikitolewa na vituo vyote vya afya nchini kuanzia ngazi ya vituo vya afya, Hospitali za Wilaya, Hospitali za Rufani za Mikoa na Kanda na Hospitali Maalum.

Katika mkakati wa kuboresha huduma hizi, serikali imeendelea kuvijengea uwezo vituo vya kutolea huduma za afya ya msingi kwa kuboresha miundombinu na vifaa tiba, kuwajengea uwezo watoa huduma za afya kuwatambua, kuwaibua na kuwahudumia wagonjwa wa shinikizo la juu la damu.


Hata hivyo, mpango wa serikali kupitia Wizara ya Afya ni kutoa mafunzo ya utoaji wa huduma za magonjwa yasiyoambukiza ikiwamo huduma za ugonjwa wa shinikizo la damu kwa watoa huduma 2,400 kutoka vituo vya afya vyote 600 katika mikoa yote 26.

Kwa mujibu wa Wizara ya Afya, mpaka sasa wizara imekwishatoa mafunzo hayo kwa jumla ya watoa huduma 1,972 kutoka mikoa 19 kati ya mikoa 26 ambayo ni sawa na asilimia 73, yanatarajiwa kukamilika kufikia mwezi Juni, 2023 na wizara imetoa vifaa vya utambuzi wa awali vya magonjwa hayo kwa vituo vya afya kwenye mikoa hiyo.

Pia serikali imeruhusu dawa za kukabili shinikizo la juu la damu katika ngazi ya msingi kwa kuruhusu dawa tatu kutumika katika ngazi ya kituo cha afya na dawa mbili kutumika katika ngazi ya zahanati.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Hili linalowakuta kwenye daladala Mwanza, sote tuwajibike kuwatetea

Na Anthony Gervas, Mwanza

**KILA** mtu tunafahamu kuwa 'elimu ni msingi wa maisha' kauli mbiu iliyobeba ujumbe wa mambo mengi, ikiwamo shughuli za kiuchumi, biashara, siasa pamoja na fursa zingine mbalimbali muhimu kitaifa.

Katika mkoa wa Mwanza, wiki hii jicho la Nipashe lilitupia macho kwa wanafunzi wa shule za sekondari za serikali, baadhi yao wanakabiliwa na mateso makubwa ya usafiri wa magari ya daladala kwenye vituo hivyo, asubuhi wakati wa kwenda shule na jioni kurudi nyumbani.

Mateso hayo yanatokana na makondakta na madereva wa magari hayo wanaogoma kuwabeba, kwa nauli ya shilingi 200 kiwango kilichopangwa na mamalaka za serikali, badala yake wakilazimika kulipa nauli ya shilingi 400 hadi shilingi 500 kiwango cha watu wazima.

Imekuwa changamoto kubwa ambayo wanafunzi hao wakati mwingine hujikuta wakikaa muda mrefu kwenye vituo vya daladala, wakihangaikia usafiri huo kwenda shule au wakati wa kurudi nyumbani, mateso hayo yanashuhudiwa kila siku katika jiji hili la Mwanza, huku baadhi ya wanafunzi wakilalamikia hali hiyo kuwavuruga kisaikolojia.

Dai kubwa la makondakta na madereva kugomea kuwabeba kwa nauli hiyo, ni kwamba wao wamepangiwa kiwango cha kupeleka makusanyo kwa tajiri mwenye gari, hivyo wanapobeba wanafunzi pesa za mawasilisho yake hupungua na kujikuta wakikosa hata posho zao za siku, halafu mmiliki anaweza kuwadai kiasi cha fedha zilizopelea wafidie.

Hali hiyo inaweza kuhatarisha maisha ya wanafunzi hawa, kwani wengi wao wanaweza kukata tamaa kuendelea na masomo au kujiingiza kwenye makundi hatarishi ikiwamo uvutaji wa dawa za kulevya, vijana wa kike kurubuniwa na wenye magari binafsi ili kupewa lifti, kupewa fedha na kupata mimba wakiwa shuleni.

Wazazi, walezi na serikali tunatakiwa kuchukua hatua mapema kulitazama suala hilo, kabla halijaleta madhara makubwa, tusilifanyie mzaha, kwani likatugharimu zaidi hapo baadaye tutabaki kunyosheana vidole, huo ni mzigo wetu tunaotakiwa kuubeba sote pamoja kutafuta ufumbuzi wake, vinginevyo tutajikuta tunazalisha taifa lenye wasomi butu waliojaa elimu viraka.

Pamoja na huruma ya serikali kuwa mwanafunzi wa kike akipata mimba akiwa shuleni, baada ya kujifungua arudi shule kuendela na masomo, jambo hilo halina afya sana sababu bila kuchukua hatua madhubuti kudhibiti changamoto hiyo mwisho wa siku taifa litakuwa linaendelea kuazalisha wanafunzi na wasomi wasio na sifa katika viwango vya elimu.

Tujue binti akishazaa mtoto akiwa shuleni tabia hubadilika kuwa za kimama au mzazi fikri zinakuwa pengine za kulea mwanaye anaporudi nyumbani, lakini haitoshi anaweza kuwaharibu kitabia hata wananfunzi wengine wa kike, kujiingiza kwenye vitendo vya mapenzi wangali wadogo,tunatakiwa kutafakari zaidi,mwisho wa siku taifa litajaa wasomi kicheko duniani.

Ni kweli, hata Ofisa Elimu Mkoa wa Mwanza, Martin Nkwabi, anakiri wanafunzi wanazuiliwa na wenye magari ya daladala kupanda hapa jijini Mwanza, asubuhi wakati wa kwenda shule na kurudi nyumbani jioni.

Anasema hali hiyo inatokanana na madai kwamba nauli wanayolipa wanafunzi shilingi 200 ni kidogo, kwani wao wamepangiwa kiwango kikubwa cha kuwasilisha pesa kwa mmiliki wa gari kila siku.

Nkwabi anasema kuna haja ya serikali kupitia mamlaka husika za utoaji viwango vya nauli kulitafutia ufumbuzi suala hilo ili wanafunzi hao waweze kupata huduma hiyo bila usumbufu,ili kuepuka changamoto zingine zinazoweza kuwakabili .

Hivyo, suala hili lisipuuzwe na mamlaka husika kwani ni hatari likiachwa bila ufumbuzi,hata kama uchungu wa mwana aujuae mzazi, zigo hili la wanafunzi ni letu sote tumeachiwa na wenye daladala hivyo tunatakiwa kulibeba ili kuokoa sekta ya elimu nchini.

# NBC yakabidhi gawio la Bil. 20/- kwa wanahisa, serikali

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imepokea Sh. bilioni sita kutoka Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) ikiwa ni sehemu ya gawio la bilioni 20 ambalo benki imetenga kwa ajili ya wanahisa wake kufuatia faida iliyopata mwaka 2022. Serikali inamiliki asilimia 30 ya hisa za benki hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, alikabidhi gawio hilo kwa Msajili wa Hazina, Nehemiah Mchechu, aliyeiwakilisha serikali wakati hafla fupi ya makabidhiano hayo iliyofanyika jana jijini Dar es Salaam. Ilihudhuriwa na wadau mbalimbali kutoka serikali na maofisa waandamizi wa benki hiyo.

Akizungumza wakati wa hafla, Mchechu, mbali na kuipongeza benki hiyo kwa mafanikio makubwa iliyoyapata katika kipindi cha mwaka 2022, aliwasilisha salamu za Rais Samia Suluhu Hassan, alitoa wito kwa taasisi na mashirika yenye umiliki wa umma kuhakikisha yanatimiza wajibu wao wa kuwasilisha gawio litokanalo na faida za uendeshaji wa shughuli zao kwa serikali.

"Serikali inafurahishwa na utendaji ulioimarika wa Benki ya NBC. Sisi kama wanahisa, tunafurahi kuona uwekezaji wetu unatoa matunda. Gawio la Sh. bilioni sita ambalo serikali inalipokea leo (jana), litaongeza ukubwa wa kapu letu la makusanyo ambayo yamekuwa yanaelekezwa katika kufanikisha miradi mbalimbali ya maendeleo hususani ile ya kimkakati. Hivyo, ninaipongeza sana Benki ya NBC kwa mafanikio haya...hongereni sana," alisema Mchechu.

Alitumia fursa hiyo kuwasilisha agizo la Rais Samia kuyataka mashirika na taasisi zingine zenye umiliki wa umma kuhakikisha zinatimiza wajibu wao wa msingi wa kuwasilisha gawio kwa serikali.

"Anachosisitiza Mheshimiwa Rais katika hili ni kwa taasisi hizi kutimiza wajibu huu kwa fedha zitokanazo na faida iliyopatikana tu na si kwa taasisi hizi kukopa mahali popote ili kulipa gawio. Taasisi zitakazoshindwa kutimiza wajibu, ipo haja ya viongozi wa taasisi hizi kujitafakari ili kuona kama kweli wanastahili kuendelea kuongoza taasisi zisizotengeneza faida kwa taifa," alisema.


Akizungumza katika hafla hiyo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya NBC, Dk. Elirehema Doriye, alisema mafanikio na mwenendo chanya wa benki hiyo unathibitisha imani kubwa waliyonayo wateja kwa benki.

"Tuna furaha kusalia katika dhamira yetu ya kufikia malengo yetu muhimu katika kupanua nyayo zetu na kuwekeza katika teknolojia ili kuboresha uzoefu wa wateja wetu. Faida yetu ya kabla ya kodi ilikuwa kwa asilimia 36 hadi Sh. bilioni 81.9 kutoka Sh. bilioni 60 mwezi Desemba 2021.

"Ongezeko hili la faida ndilo linatuwezesha kutoa Sh. bilioni 20 kama gawio kwa wanahisa wetu. Leo (jana) tunafurahi kukabidhi hundi ya Sh. bilioni sita kama gawio kwa mwaka 2022. Tunatazamia mustakabali wenye matumaini zaidi huku pia tukiwa tunaendelea kutoa huduma bora zaidi kwa wateja wetu," alisema Doriye.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, aliishukuru serikali kwa kuweka mazingira mazuri kwa taasisi za fedha kama Benki ya NBC kustawi huku pia akiipongeza Bodi ya Wakurugenzi wa benki hiyo pamoja na wafanyakazi kwa jitihada kubwa walizofanya hadi kufikia mafanikio hayo.

"Benki ya NBC ndiyo mdhamini mkuu wa Ligi Kuu ya Soka Tanzania Bara, ambayo inazalisha ajira na kusaidia uwezeshaji na ushirikishwaji wa kifedha." alsiema Sabi huku akibainisha kuwa benki hiyo iliongeza matawi matano mapya katika kipindi cha mwaka wa 2022 huku wakala wa mtandao wa benki hiyo ukikua kwa asilimia 82 kutoka mawakala 5,121 hadi 9,525.




Msajili wa Hazina, Nehemiah Mchechu (katikati), akipokea mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. bilioni 6 kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (kushoto), ikiwa gawio la mwaka 2022 kwa serikali inayomiliki asilimia 30 ya hisa za benki hiyo, jijini Dar es Salaam jana. Wanaoshuhudia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa benki hiyo, Dk. Elirehema Doriye (wa pili kushoto) pamoja na maofisa waandamizi wa Ofisi ya Msajili wa Hazina. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jaji awa kikwazo kesi kina Mdee

**Na Grace Gurisha**

KESI ya kupinga kuvuliwa uanachama iliyofunguliwa na wabunge 19 wa Viti Maalum kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), imeahirishwa kusikilizwa hadi Julai 10 na 11 mwaka huu kutokana na jaji anayeisikiliza kuwa na vikao vya mahakama.

Kesi hiyo ilitarajiwa kusikilizwa jana mbele ya Jaji Cyprian Mkeha wa Mahakama Kuu, Masjala Kuu Dar es Salaam kwa hatua ya mjumbe wa Bodi ya Wadhamini wa Chama hicho, Lucy Mollel, kuulizwa maswali ya dodoso na mawakili wa wabunge hao.

Kutokana na jaji kutokuwapo, Kaimu Msajili wa Mahakama hiyo, Veronica Mteta, aliahirisha kesi hiyo hadi tarehe hizo kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa.

Mollel anatarajia kuulizwa maswali hayo kutokana na kiapo kinzani alichokiwasilisha mahakamani baada ya Mbunge wa Viti Maalum, Halima Mdee na wenzake 18 kufungua kesi kupinga kuvuliwa uanachama na chama hicho.

Machi 6, mwaka huu, Wakili wa Waleta Maombi, Ipilinga Panya, aliiomba mahakama itoe hati za wito za wajumbe saba wa bodi hiyo ili waje mahakamani kujibu maswali ya dodoso kuhusiana na viapo vyao kinzani katika maombi hayo.

Panya aliwataja wajumbe hao kuwa ni Silvester Masinde, Profesa Azaveri Lwaitama, Lucy Mollel, Mary Joakim, Francis Mushi, Maulida Komu na Ahmed Hamis, ambao wanataka kuwahoji kutokana ana vitu ambavyo wamevieleza katika kiapo kinzani cha CHADEMA.

Mbali Panya, mawakili wengine ni Aliko Mwamanenge, Edson Kilatu, Emmanuel Ukashu, Joyce Mwakakila na Afrey Maunga. Kwa upande wa wajibu maombi, wapo Wakili Peter Kibatala na Jeremiah Mtobesya.

Mdee na wenzake walifungua shauri hilo namba 36/2022 la Julai 22, 2022, wakiomba mahakama ipitie mchakato na uamuzi wa kuwafukuza uanachama na kisha itoe amri tatu.

Katika shauri hilo, wabunge hao wanaiomba mahakama itengue mchakato na uamuzi wa kuwavua uanachama na pia iwalazimishe CHADEMA kuwapa haki ya kuwasikiliza.

Pia wanaomba kuwekwa zuio kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuchukua hatua yoyote hadi malalamiko yao yatakapotolewa uamuzi.

## KABWELA

**Na Fadhil Mohammed**



# Mabula amulika weledi madalali wa Mabaraza ya Ardhi, Nyumba

**Na Munir Shemweta,** DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameitaka Kamati ya Uteuzi na Nidhamu ya Madalali na Wasambaza Nyaraka wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kuhakikisha madalali wanaoteuliwa, wanapata mafunzo na wenye weledi wanaoweza kufanya kazi kwa staha.

Dk. Mabula aliagiza hayo juzi alipokutana na Kamati ya Uteuzi na Nidhamu ya Madalali na Wasambaza Nyaraka wa Mabaraza ya Ardhi, Nyumba na Wilaya ilipokwenda kumtembelea ofisini kwake Mtumba jijini hapa.

Kamati hiyo ambayo iko chini ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, iliundwa Desemba 27, 2021 kwa mujibu wa kifungu cha 2&3 cha Sheria ya Mahakama za Migogoro ya Ardhi Sura 216.

"Ni vizuri madalali mtakaowateua waonekane ni wale waliopata mafunzo na wenye weledi na wanaoweza kufanya kazi kwa staha. Hilo nalo ni zuri zaidi.

"Unakwenda kutekeleza amri ya mahakama halafu unachukua vitu unarusha huko. Hiyo hapana! Tunatambua ni amri ya mahakama lakini basi ifanyike kwa staha, siyo kujivurugia kwa sababu ni dalali, tusingependa kuingia kwenye historia ya kuanza na madalali walioteuliwa kwa kanuni mpya na kupigiwa kelele," aliagiza Dk. Mabula.

Waziri huyo pia aliwataka madalali walio na leseni za utekelezaji kutokwenda moja kwa moja katika tukio bila kupita ofisi za utawala wa eneo husika na kutaka madalali wakati wa utekelezaji kupita kwa Mkuu wa Mkoa, Wilaya au Ofisa Tarafa kutegemeana na utaratibu utakaowekwa ili kazi ifanyike kwa baraka za utawala.

"Kumekuwa na changamoto hiyo mara nyingi sana. Dalali anapata kazi, anaamkia eneo la tukio. Anakwenda kuvunja nyumba. Mimi nisingependa yatokee kwa staili hiyo. Ni vizuri kupita kwa Mkuu wa Wilaya, akaona hukumu yenyewe au amri ya mahakama na kujiridhisha ingawa hana namna ya kubadilisha, lakini akawa na taarifa nini kinakwenda kufanyika," alisisitiza.

Pia alizungumzia suala la wito wa mahakama, akitoa msisitizo kujua sheria inasemaje kwa mtu anayepelekewa wito na kukosekana mara moja au mbili nyumbani kwake.

"Nisingependa malalamiko yatokane na madalali walioteuliwa halafu mtu akose haki kutokana na kutopata wito au nyaraka iliyotoka mahakamani na taratibu nyingine zikaendelea.

"Ni vizuri kuangalia utaratibu mzuri wa kuhakikisha mhusika amefikiwa na kama hakufikiwa, utaratibu upi unatumika ili walau afahamishwe kile kinachoendelea. Vinginevyo tunatumia madalali badala ya kupunguza changamoto zinakuwa zinaendelea," alisema.

Majukumu makuu ya Kamati ya Uteuzi na Nidhamu ya Madalali na Wasambaza Nyaraka wa Mabaraza ya Ardhi ni kufanya uteuzi wa Madalali na Wasambaza Nyaraka wa Mabaraza ya Ardhi, kusikiliza na kuamua madai ya utovu wa nidhamu dhidi ya madalali na wasambaza nyaraka wa mabaraza ya ardhi pamoja na kuunda na kusimamia kamati ndogo za kusimamia madalali na wasambaza nyaraka katika ngazi za mikoa.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Standard Chartered, Herman Kasekende, akizungumza wakati wa uzinduzi wa toleo jipya la mfumo wa kibenki wa kidigitali uitwao 'Straight2bank Next Gen', jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Kesi ya nyara za serikali yafutwa

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, imefuta kesi namba 53/2022 ya nyara za serikali (meno ya tembo), baada ya upande wa mashtaka kung'ang'ania kuwa mshtakiwa, Abubakari Msawa, aliandika barua ya makubaliano (plea bargaining) wakati mwenyewe anadai hajawahi kufanya hivyo.

Aidha, mahakama hiyo imesema imefikia uamuzi huo kwa sababu kesi hiyo imeahirishwa mara ya sita kusikilizwa kwa madai ya upande wa mashtaka wanashughulikia barua ya 'plea bargaining' ya mshtakiwa.

Uamuzi huo ulitolewa juzi na Hakimu Mkazi Mkuu, Richard Kabate, wakati kesi hiyo ilipoitwa kwa ajili ya kusikilizwa kwa mashahidi wa upande wa mashtaka, lakini Wakili wa Serikali, Agness Mtunguja, alidai kuwa bado wanaendelea kushughulikia barua hiyo.

"Msawa naomba utuondolee utata huu kwa sababu kesi imeshindwa kusikilizwa kutokana na kumbukumbu kuwa wewe unataka kukiri kosa ili upate adhabu ndogo," aliuliza Hakimu Kabate.

Akijibu swali hilo, Mshtakiwa Msawa alidai kuwa tarehe iliyopita Wakili Mtunguja akiwa na mwenzake aliwaeleza kuwa hajawahi kuandika barua hiyo, lakini anashangaa upande wa mashtaka unavyong'ang'ania hivyo.

"Kama ningeandika barua hiyo mheshimiwa hakimu ungepata nakala hiyo kwenye jalada lako, tangu mwaka 2018 nipo gerezani imekuwa wimbo ni ule ule tu, mimi sijaandika barua yoyote," alidai Msawa.

Baada ya Msawa kudai hivyo, Hakimu Kabate alisema upande wa mashtaka ndiyo waliitaarifu mahakama kuwa kuna plea bargaining, lakini mshtakiwa alikataa, kesi imeahirishwa mara kadhaa kwa sababu hiyo.

# Wanahisa benki waitwa kujadili maslahi

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

BENKI ya CRDB inatarajia kufanya Mkutano Mkuu wa 28 wa Wanahisa Jumamosi katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC).

Mkutano huo unafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Kampuni Na. 212 ya Mwaka 2002. Kila mwaka Benki ya CRDB imekuwa ikiandaa mkutano huo unaowapa wanahisa fursa ya kujadili masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupitisha au kuidhinisha uamuzi mbalimbali wenye maslahi kwa benki.

Akizungumza katika mkutano na waandishi wa habari uliofanyika Hoteli ya Mount Meru jijini Arusha juzi, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Benki ya CRDB, Dk. Ally Laay, alisema mkutano huo utafanyika kwa njia mseto (Hybrid Meeting) ili kutoa fursa kwa wanahisa wengi zaidi kushiriki kwa njia ya kidijitali.

Dk. Laay alisema kuwa katika Mkutano Mkuu wa 27 wa Wanahisa waliadhimia Mkutano wa 28 ufanyike Makao Makuu ya Benki ya CRDB jijini Dar es Salaam, lakini kwa kuzingatia mkakati mpya wa benki wa 2023-2027, Bodi ya Wakurugenzi ilipitia na kuidhinisha mabadiliko ya eneo la mkutano kwenda AICC.

"Bodi ya Wakurugenzi ilipendekeza mabadiliko hayo ya sehemu ya kufanyika Mkutano Mkuu kwa wanahisa wanaomiliki zaidi ya asilimia 50 kulingana na Katiba na Mkataba wa Benki (MEMARTS) na Sheria ya Kampuni Na. 12 ya 2002, na wanahisa walikubali mabadiliko haya," alisema Dk. Laay huku akiwakaribisha wanahisa katika mkutano huo.

Dk. Laay alisema mkutano huo pia utafanyika kupitia mtandaoni. Wanahisa watajiunga kuanzia saa 2:00 asubuhi kupitia mtandao au kupitia SimBanking App. Imewekwa sehemu ya kujisajili kushiriki Mkutano Mkuu.

"Tumeweka mwongozo wa jinsi ya kushiriki mkutano mkuu kwa njia ya mtandao kupitia tovuti yetu rasmi, mitandao yetu ya kijamii, lakini pia maelekezo yametumwa kwa ujumbe mfupi kwa wanahisa," alisema Dk. Laay huku akiwahakikishia kuwa watashiriki bila changamoto yoyote.

Mkutano Mkuu wa 28 wa Wanahisa wa Benki ya CRDB utatanguliwa na semina maalum kwa wanahisa na umma yenye kaulimbiu ya 'Ushirika wa Serikali na Benki ya CRDB kuwezesha Vijana na Wanawake kupitia Programu ya IMBEJU'. Semina hiyo ambayo pia itaambatana na maonyesho ya vijana wabunifu, itafanyika kesho kuanzia saa 3 asubuhi katika ukumbini AICC.

Mgeni Rasmi katika semina hiyo anatarajiwa kuwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mwigulu Nchemba, mada mbalimbali zikiwasilishwa na wataalamu wa masuala ya fedha, sheria na uwekezaji katika masoko ya mitaji.

Ajenda zitakazojadiliwa katika Mkutano Mkuu wa 28 wa Wanahisa wa Benki ya CRDB ni pamoja na uchaguzi wa wajumbe huru wa bodi, kuteua wakaguzi wa hesabu na kujadili na kupokea Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi na Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa na gawio kwa mwaka 2022. Pendekezo la gawio la Sh. 45 kwa hisa litawasilishwa.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya CRDB, alisema pendekeo hilo la ongezeko la gawio kwa hisa linatokana na Benki ya CRDB kuendelea kupata matokeo mazuri sokoni ambapo mwaka wa fedha ulioisha ilipata faida baada ya kodi ya Sh. bilioni 351.4 kulinganisha na Sh. bilioni 268 mwaka 2021.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema kuwa katika Mkutano Mkuu wa 28, wanahisa watapata nafasi ya kujadili mkakati mpya wa biashara wa muda wa kati wa miaka mitano 2023 - 2027.

Nsekela alitumia fursa hiyo kuwahamasisha wanahisa wa Benki ya CRDB kujitokeza kwa wingi kwa kuwa ushiriki wao utaiwezesha Bodi na Menejiment kupata maoni yao ya namna bora ya kuboresha utendaji.

# Watoto 130 wagundulika kuwa na maambukizi ya VVU

**Na Dege Masoli,** KILINDI

WATOTO 130 wenye umri wa chini ya miaka 15 waliopima afya wamegundulika kuwa na maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) na kuanzishiwa huduma ya kutumia dawa za kufubaza makali ya ugonjwa huo.

Taarifa kuhusu hali hiyo ilielezwa jana na Mwenyekiti wa Kamati ya Ukimwi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi, mkoani Tanga, Amon Ramadhan, alipowasilisha ripoti hiyo kwenye baraza la madiwani.

Kwa mujibu wa Amon, watoto hao ni kati ya watu 1, 849 wanaoapata dawa za kufubaza VVU kwenye vituo 38 vya kutolea huduma hiyo.

"Watoto hao wakiume ni 60 na wa kike 70 ambao ni sawa na asilimia saba ya wateja wote, kinamama wajawazito ni 35 na wanaonyonyesha ni 95....wateja wote hawa pia wamefanyiwa tathmini ya maambukizi ya kifua kikuu na kupatiwa huduma," alieleza Amon.

Hata hivyo, alieleza kuwa kwa kipindi cha kuanzia Januari hadi Machi mwaka huu jumla ya watu 7044 walipima afya zao kwenye vituo vya kutolea huduma hiyo na 96 kati yao walikutwa na maambukizi wakiwamo wajawazito 10 kati ya 3,091 waliopima.

Aidha kwa upande wa magonjwa yanayotokana na ngono, mwenyekiti huyo alieleza kuwa kwa kipindi hicho jumla ya wagonjwa 849 wamehudhuria na kupata matibabu.

Aliyataja magonjwa hayo ni kisonono wagonjwa 319, vidonda vya tumbo 79, matatizo ya tumbo kwa wanawake 272 na magonjwa mengine ni watu 179.

**Watoto hao wakiume ni 60 na wa kike 70 ambao ni sawa na asilimia saba ya wateja wote, kinamama wajawazito ni 35 na wanaonyonyesha ni 95.... wateja wote hawa pia wamefanyiwa tathmini ya maambukizi ya kifua kikuu na kupatiwa huduma.**

# Mahakama yatupa maombi ya Jamhuri kesi ya Loliondo

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Arusha imetupilia mbali pingamizi la kisheria lililowekwa na Jamhuri katika kesi ya wananchi wa Loliondo, wanaopinga ardhi waliyokuwa wakiishi kwa miaka mingi kutangazwa kuwa Pori Tengefu la Pololeti.

Ardhi hiyo iliyotangazwa na Waziri wa Maliasili na Utalii, kuwa Pori Tengefu la Pololeti iko Wilaya ya Ngorongoro, mkoani Arusha na ina ukubwa wa kilometa za mraba 1,502.

Akisoma uamuzi mdogo jana kuhusu shauri hilo, Jaji Joachim Tiganga, alisema mahakama hiyo imeamua kutupilia mbali pingamizi hilo baada ya Jamhuri kushindwa kujenga hoja yao katika pingamizi ililoweka ili kuondoa shaka.

Katika pingamizi hilo, Jaji Tiganga, alisema Jamhuri iliwasilisha mahakamani humo pingamizi lake, ikipinga upande wa waleta maombi ulichelewesha jalada la kesi hiyo, hivyo kesi hiyo ilifunguliwa nje ya muda.

**Tatu, wananchi hao wanaiomba Mahakama hiyo itamke kuzuia serikali na mawakala wake wasifanye operesheni yoyote kwenye eneo hilo.**

Baada ya kumaliza kusoma uamuzi huo, Jaji Tiganga, aliahirisha kesi hiyo hadi Mei 29, mwaka huu, wakati mahakama hiyo itakapoanza rasmi kusikiliza shauri hilo.

Akizungumza nje ya mahakama hiyo, wakili anayeongoza jopo la utetezi, Denis Mosess, alidai kuwa uamuzi huo wa Mahakama umezingatia haki, hivyo sasa wapo tayari kwa ajili ya kusikiliza kesi hiyo tarehe iliyopangwa na Mahakama.

Mawakili wengine katika jopo hilo la utetezi ni Joseph Shangay na Yonas Masiaya, wakati mawakili wa Jamhuri wanaongozwa na Jackline Kinyasi akisaidiwa na Charles Mtahe.

Katika shauri hilo, waleta maombi watano katika kesi hiyo kutoka vijiji vilivyoathirika, wanaiomba Mahakama iagize serikali kuondoa zuio dhidi ya wananchi kuingia kwenye eneo la kilomita 2 1,502 ambalo wamekuwa wakitumia kwa ajili ya malisho ya mifugo yao na kufanyia shughuli za imani yao.

Pili, wanaiomba Mahakama itengue Tangazo la Serikali (GN 421) la Juni 17, 2022, kwamba ni batili na lilitangazwa kinyume na sheria na halikuwashirikisha wananchi kama sheria inavyotaka.

Tatu, wananchi hao wanaiomba Mahakama hiyo itamke kuzuia serikali na mawakala wake wasifanye operesheni yoyote kwenye eneo hilo.

Jamhuri katika kesi hiyo ikiongozwa na wakili Jackline Kinyasi, inadai kuwa imeweka pingamizi hilo kwa kuwa upande wa utetezi haukuwasilisha jalada la kesi hiyo katika muda muafaka, hivyo walikuwa nje ya muda.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako (wa pili kulia), akiangalia bidhaa mbalimbali alipotembelea maonyesho ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Marekani, China zaonyesha nia kununua kahawa Tanzania

**Na Godfrey Mushi,** HAI

WAFANYABIASHARA wakubwa wa kahawa kutoka Marekani na China, wameonyesha nia ya kununua kahawa ya Tanzania kupitia Chama cha Ushirika wa Mazao cha Lukani/Losaa Amcos Ltd kilichoko Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro.

Akiwasilisha taarifa ya mauzo ya kahawa kwa mwaka 2022/23 wakati wa mkutano mkuu wa mwaka uliofanyika jana, Mwenyekiti wa Lukani/Losaa Amcos Ltd, Ebenetho Munuo, alisema kampuni ya Marekani iliyoonyesha nia hiyo ni Rafiki Coffee Ltd na Mteja Crop to Cup.

"Kwa msimu huu tumekuwa na tatizo la kibiashara kwa soko la nje, kwani mteja wetu Kampuni ya Kyowas haikuongeza oda, lakini pamoja na juhudi kubwa iliyofanywa na bodi ya chama kukusanya kahawa, bei ya soko la ndani la kahawa ilishuka toka Dola za Marekani 260 hadi Dola za Marekani 160 kwa gunia la daraja AA, tofauti na msimu uliopita.

Hii ilifanya wakulima kulipwa shilingi 6,500 kwa kilogramu ya kahawa kavu na shilingi 9,000 kahawa kavu kutoka kiwandani ikiwa imekobolewa. Tuliweza kuuza kahawa nje ya nchi kule Japan, gunia 140 za kilogramu 60 kwa Dola za Marekani 285," alisema.

Aidha, Munuo, alisema kwa msimu wa mwaka 2022/23 vijiji vya Lukani/Losaa, vilipokea Dola za Marekani 6,000 sawa na zaidi ya Sh. milioni 13.9 kwa ajili ya maendeleo ya jamii.

"Bodi inaomba pesa zitakazopewa vijiji vyetu zitumike kwa kuchangia maendeleo ya jamii yaliyoibuliwa na wananchi. Kwa msimu wa 2023/24 vitapokea Dola za Marekani 2,000 kama ilivyo katika mkataba na mwekezaji wa shamba letu la Boloti." alisema.

Kuhusu kujenga uwezo kwa vijana kulima kahawa, alisema tayari bodi ya chama hicho imeunda kikundi cha vijana maarufu VIKATA, ambacho kimesajiliwa kwa ajili ya kuzalisha kahawa na tayari kahawa yao iko kwenye matangazo nchini Japan.

"Msimu huu tayari tumeshawagawia wakulima miche zaidi ya 67,000. Hiyo ni pamoja na aina mpya ya miche bora ya compact kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania (TaCRI).

Alisema Bodi ya Kahawa Tanzania (TCB), imehidi kukipa chama hicho ruzuku ya miche 16,000 ambayo ni sawa na Sh. milioni 4.8.



# Sababu ongezeko la plastiki katika Ziwa Victoria zatajwa

**Na Vitus Audax,** MWANZA

ZIWA Victoria ni sehemu ya janga la uchafuzi wa plastiki huku wataalamu wakisema chupa za plastiki za maji ya kunywa milioni moja hununuliwa kila dakika na mifuko trilioni tano ya plastiki hutumika kila mwaka.

Aidha, tani milioni za plastiki huingizwa katika maji ulimwenguni kila mwaka na kuyaweka hatarini maisha ya viumbe hai wanaoishi majini, ambao ni pamoja na samaki.

Nipashe ilitembelea baadhi ya maeneo ya mialo iliyopo mkoani Mwanza na kubaini hali ya uchafuzi wa Ziwa Victoria inayofanywa na wavuvi pamoja na wafanyabiashara huku uchafu mwingi ukiwa ni wa mifuko na chupa za plastiki wakieleza kuwa hali hiyo husababishwa na ongezeko la watu katika eneo hilo ambalo halina sehemu rasmi ya kumwaga taka.

Abdullahaziz Shabani, mvuvi katika Mwalo wa Mswahili, alisema katika mwalo huo hukusanya taka zao katika eneo la karibu na ziwa hilo na kutokana na wingi wa wafanyabiashara pamoja na wavuvi katika eneo hilo taka zimeongezeka na kuingia ziwani hali inayohatarisha afya zao na viumbe wa majini.

**Ni kosa kisheria kuweka dampo la taka katika eneo la chanzo chochote cha maji na kwa wanaogundulika kufanya hivyo huchukuliwa taratibu zote za kisheria kukomesha uchafuzi wa aina hiyo.**

Aidha, aliwaomba wadau wa mazingira pamoja na mamlaka husika kupambana na kudhibiti hali hiyo ili kurejesha mialo pamoja na ziwa katika hali ya usalama.

Akizungumza na Nipashe kuhusu wajibu wa wadau mbalimbali wa mazingira katika kudhibiti uchavuzi wa plastiki katika Ziwa Victoria na vyanzo vingine vya maji, Mratibu Mkuu wa Shirika la Synergistic Globe, Angelina Manyama, alisema elimu kwa watumiaji na watu wa jirani na vyanzo hivyo ndilo suala la muhimu.

"Elimu hiyo inatakiwa kutolewa kwa watu wote hususan waliopo karibu na mitaro inayotiririsha maji katika vyanzo vikuu vya maji, kwa wafanyabiashara na wavuvi wanaofanya shughuli zao katika Ziwa Victoria kuhakikisha wanatunza ziwa hilo," alisema Manyama.

Mkurugenzi wa Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria, Renatus Shinhu, akieleza mikakati ya bodi hiyo kuhusu udhibiti wa uchafuzi wa Ziwa Victoria kupitia shughuli za kibinadamu, alisema jukumu la utunzaji wa vyanzo vya maji ni la kila mwananchi.

Alisema watumishi wa bodi hiyo kwa kushirikiana na watumiaji pamoja na watu wanaofanya shughuli zao karibu na vyanzo vya maji uhakikisha wanafanya usafi katika Ziwa Victoria kwa kuondoa taka ngumu zikiwamo plastiki pamoja na gugumaji ambazo sambamba na kuelimisha juu ya utunzaji na athari za uchavuzi wa vyanzo maji.

Aidha, alisema kuwa ni kosa kisheria kuweka dampo la taka katika eneo la chanzo chochote cha maji na kwa wanaogundulika kufanya hivyo huchukuliwa taratibu zote za kisheria kukomesha uchafuzi wa aina hiyo.



Mkuu wa Wilaya ya Serengeti, Dk. Vincent Mashinji (wa nne kushoto), akikabidhi majiko ya gesi kwa wawakilishi wa walimu zaidi ya 1,750 kutoka katika shule za sekondari na msingi 190 za wilaya hiyo, mkoani Mara juzi, yaliyotolewa na Rhimo Nyansaho kupitia Taifa Gesi kwa lengo la kuhimiza utunzaji mazingira na kuokoa muda wa walimu wawapo shuleni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Shirika lawapatia bima ya afya watoto wa mitaani

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WATOTO 30 ambao walikuwa wakiishi mitaani na kurejeshwa katika familia zao katika Manispaa ya Shinyanga wamekatiwa bima ya afya.

Kadi hizo wamekatiwa juzi na Taasisi ya Nancy Foundation ambayo ndiyo imekuwa ikitekeleza mradi wa kuwaondoa watoto wanaoishi mitaani katika Manispaa ya Shinyanga na kuwarudisha majumbani kwao.

Dk. Martine Masalu kutoka Hospitali ya Rufani mkoani Shinyanga, akizungumza kwa niaba ya Taasisi ya Nancy Foundation, alisema suala la afya ni muhimu na ndiyo maana taasisi hiyo imeamua kuwakatia bima ya afya watoto hao ambayo itakuwa msaada katika kuokoa afya zao.

Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Ezra Manjerenga, alisema kadi hizo za CHF zitakuwa pia msaada kwa familia nzima ya watoto hao kwa kupata huduma ya matibabu bure.

Aidha, alisema licha ya watoto hao kuwakatia bima ya afya watawalipia pia huduma ya chakula shuleni, masomo ya ziada ili wasome katika mazingira rafiki, pamoja na kuona namna ya kuinua uchumi wa familia zao.

Baadhi ya wazazi wa watoto hao akiwamo Farida Kasigwa, waliishukuru taasisi hiyo kwa kuwasaidia kuwatoa watoto wao kuishi mitaani.

**Licha ya watoto hao kuwakatia bima ya afya watawalipia pia huduma ya chakula shuleni, masomo ya ziada ili wasome katika mazingira rafiki, pamoja na kuona namna ya kuinua uchumi wa familia zao.**

# Benki ya Dunia yatoa bil. 31/- ujenzi barabara Mwanza

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

BENKI ya Dunia (WB) imetoa Sh. bilioni 31.3 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara kwa kiwango cha lami, ikiwamo ujenzi wa Soko la Mwaloni Kirumba, katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, jijini hapa.

Kwa mujibu wa Mstahiki Meya wa manispaa hiyo, Renatus Mulunga, barabara zitakazojengwa ni kutoka Buswelu-Mbogamboga kupitia Nyamadoke hadi stendi kuu ya mabasi Nyamhongolo, zenye urefu wa kilomita 9.7 ambazo zitagharimu Sh. bilioni 16.2.

Alitaja barabara zingine ni kutoka Buswelu mzunguko hadi mnada wa mbuzi, Igoma zitakazogharimu Sh. bilioni 4.1 zenye urefu wa kilomita 3.3, Barabara za Kirumba zenye urefu wa kilomita 2.9 na ujenzi wa soko la mwaloni -Kirumba lenye ghorofa, miradi itakayogharimu Sh. bilioni 11.

"Benki ya Dunia imetufadhili fedha hizo jumla ya Sh. bilioni 31.3 kwa ajili ya ujenzi wa miradi hiyo, likiwamo soko la dagaa na samaki mwaloni- Kirumba, hivi sasa hatua zinazoendelea tunafanya tathmini katika maeneo ya wananchi yanayotakiwa kulipwa fidia, alisema Mulunga.

Mulunga alisema, wanaendelea kufanya mchakato wa kumpata mkandarasi wa ujenzi wa miradi hiyo ili kufikia Julai, mwaka huu, iweze kuanza kutekelezwa na wananchi waondokane na kero zinazowakabili kutokana na huduma za miundombinu na soko hilo.

Alisisitiza umoja wa madereva wa daladala mkoani Mwanza (Mwaredda), kuacha kutishia kugoma tena Jumatatu wiki ijayo, ikiwa umoja huo umesema endapo serikali itashindwa kutekeleza ujenzi wa stendi yao kwa kiwango cha lami, watarejea katika mgomo kama kawaida.

Aliwataka kuwa karibu na ofisi ya Mstahiki Meya na Mkurugenzi wa halmashauri ya manispaa hiyo ili kutatua changamoto kwa pamoja zinazoweza kujitokeza na kuwa wavumilivu kwa kuwa serikali imechukua hatua kuhakikisha matengenezo ya muda yanafanyika kwa ajili ya huduma kuendelea.

Umoja huo wa madereva wa daladala mkoani Mwanza, uligoma kutoa huduma hizo kwa takribani saa nne wakidai miundombinu ya barabara na stendi yao ya Nyamhongolo kuwa ni mbovu, yenye mashimo, ambayo inasababisha kuharibu magari yao, lakini kwa sasa serikali imeshafukia na huduma zinaendelea kama kawaida.

ama
ALHAMISI MEI 18, 2023
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 13

## Taharuki Katavi wanyamapori kuvamia makazi wakiua, madhara hadi mali zao



## KUTOKA NG'AMBO SINGIDA... Kutanuliwa huduma maji kulivyojibu kwa mapinduzi zahanati hadi darasani

Ukurasa 13

# Utalii Tiba aliyowekeza Rais 2021, zao lake mabingwa watibu 500 Malawi

**Na Mwandishi Wetu**

KUNA dhana inayoitwa utalii tiba, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ameipa nafasi tangu aingie madarakani, Machi 2021, ikiwa ni sehemu ya mikakati kuimarisha sekta ya afya.

Ilipofika Julai mwaka huo, aliyekuwa Waziri wa Afya, Doroth Gwajima, akatoa ufafanuzi wa Utalii Tiba, akinena: "mgonjwa anachagua hospitali ambayo inatoa huduma bora na nzuri. Utalii huu unafanyika kwa Watanzania wenyewe na kwa wagonjwa wanaotoka nje ya nchi kuja kutibiwa hapa nchini."

Vilevile akiwa ziarani mkoa wa Kigoma Oktoba mwaka jana, Rais Dk. Samia akatilia mkazo kwamba mkoa utakuwa kituo kikuu cha utalii wa tiba, hatua iliyoendana na kutoa shilingi bilioni tano za ujenzi wa hospitali ya kanda- Maweni.



Mratibu wa Matibabu Nje ya Nchi kutoka Wizara ya Afya, Dk. Asha Mahita, akimkabidhi Mkurugenzi Mtendaji wa Ocean Road, Dk. Julius Mwaiselage, kitabu chenye mpango mkakati wa utalii tiba kilichoandaliwa na Kamati ya Kitaifa ya Utalii Tiba, siku chache zilizopita. **PICHA: MTANDAO.**

Rais Dk. Samia akasema serikali imeamua kuifanya Kigoma kitovu cha biashara, hivyo inaendelea kuujenga sambamba na kuboresha miundombinu ya barabara, maji, afya na elimu, kuhakikisha huduma muhimu zinapatikana.

"Sisi maono yetu tuwe na utalii wa afya, watu watoke nchi jirani waje kupata huduma za tiba hapa. Tanzania iwe kituo cha ubingwa wa mambo ya afya kwa nchi tunazopakana nazo, ndio maana nimetoa tena hizo shilingi bilioni tano, kwa ajili ya ujenzi wa hospitali mpya ya Kanda hapa Kigoma," anasema Rais Dk. Samia.

Anasema Kigoma ni mkoa ulioko pembezoni mwa nchi, sasa wameufanya mkoa wa kimkakati wa biashara, ndio maana serikali imehakikisha unapata umeme wa uhakika, ufungue fursa za uwekezaji.

Mnamo tarehe 11 mwezi huu, imezinduliwa Kamati za Utalii Tiba kutoka Hospitali za Taifa Muhimbili (MNH), Hospitali ya Mifupa Muhimbili (MOI) na Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI) uliofanyika jijini Dar es Salaam.

Kamati ya Taifa ya Utalii Tiba inayoongozwa na Profesa Mohamed Janabi, ambaye ni mkuu wa MNH, imezinduliwa, huku imeeshaanza kufanya kazi yake. Makamu wake ni Mkurugenzi Mkuu wa Global Education Link (GEL), Abdulmalik Mollel.

Hadi sasa kuna wagonjwa wanaokuja kupata matibabu nchini, ikielezwa idadi inaongezeka kila mwaka.

Madaktari bingwa wa Tanzania wamekuwa wakienda nchi jirani kutoa matibabu ya kibingwa na kutoa utaalamu kwa madaktari wenzao wa nchi jirani, mara kadhaa wakija nchini.

Sasa inarejewa na kamati, kuwa sehemu ya matunda ya uwekezaji mkubwa uliofanywa na Rais Dk. Samia, ukizama katika hospitali nyingi kitaifa, kama uzinduzi aliofanya Rais mwaka jana katika Hospitali ya Maweni, Kitovu cha Utalii Tiba.

Sasa, inatajwa uwekezaji unaowatamanisha watu wa mataifa ya jirani kufika nchini kupata matibabu badala ya kwenda jamii ilikozoea, India, Ulaya na Marekani.

Hospitali za Tanzania kwa sasa zinatajwa kuwa na vifaa tiba vya kisasa na teknolojia, hali iliyo kivutio kikubwa kwa wagonjwa wengi kuahirisha safari za ughaibuni.

Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), sasa iko juu kwa umahiri wa kitabibu, vifaa vya teknolojia ya kisasa, ikipokea idadi kubwa ya wagonjwa kutoka nchi mbalimbali za Afrika, kuja kupata tiba.

Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Dk. Peter Kisenge, anasema kwa miaka miwili hadi sasa imepokea wagonjwa 215, kutoka nchi jirani za Afrika Mashariki na baada ya kupata matibabu, inahakikiwa si tofauti na India na Ulaya.

Kamati ya Utalii Tiba sasa ina msisitizo kuifanya Tanzania kitovu cha utalii tiba, kwa kuelezea tiba zinazopatikana nchini, vifaa tiba vilivyowekezwa na serikali na teknolojia zake.

Kwenye uzinduzi wa Kamati za Utalii tiba za hospitali nne, Profesa Janabi, akasema uwekezaji mkubwa umefanywa kwenye miundombinu ya hospitali na vifaa tiba vya kisasa unakusudia kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha utalii wa tiba kwenye ukanda wa kusini mwa Jangwa la Sahara Afrika.

Mkurugenzi wa JKCI, Dk Peter Kisenge anapongeza kamati hiyo na kusema kuwa maono ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ya kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha utalii wa tiba yanaonekana kuanza kutimia kutokana na kazi kubwa ambayo imefanywa na kamati hiyo.

Anasema mwakani JKCI inatarajia kufanya mkutano mkubwa visiwani Zanzibar, utakaihudhuriwa na zaidi ya mataifa 40 kuonyesha shughuli zinazofanywa na taasisi hiyo ili dunia ijue huduma zinazotolewa na taasisi hiyo.

"Kwa miaka mitatu JKCI imekuwa na ongezeko kubwa la wagonjwa kutoka nje ya nchi, tumeshapokea wagonjwa kutoka nchi nane. Kwa mwaka jana tu zaidi ya wagonjwa 200 walifika JKCI kutoka nje ya nchi lakini kwa mwaka huu mpaka sasa tumepata wagonjwa 110," anasema

"Sisi JKCI tumeanza safari ya kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha utalii wa tiba Afrika na tumeshapeleka madaktari wetu kwenye nchi mbalimbali kama Comoro na Malawi na tunatarajia kwenda Burundi na Congo siku chache zijazo. Tumeweka mipango ya kutekeleza maono ya Kamati ya Utalii," anase-

Inaendelea Uk. 13

MAZINGIRA

# Taharuki Katavi; wanyamapori kuvamia makazi wakiua, madhara hadi mali zao

## • Viongozi wavutana, suluhisho kitendawili ...

**Na Neema Hussein, Nsimbo**

IMEKUWA kilio endelevu sehemu mbalimbali za mkoa wa Katavi wanyamapori wakiwamo fisi, mbwamwitu na tembo wanaingilia makazi ya watu, wakiwadhuru na mali zao.

Ni shida sugu, hoja inahamia kwenye Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya Nsimbo, malalamiko ya kutaka ufumbuzi wanyama wakali kuvamia makazi ya watu kwa madhara, ikiwamo vifo vyao.

Diwani Kata ya Stalike, Adam Chalamila, analalamika katika eneo lake lililopakana na Hifadhi ya Taifa ya Katavi, kunavamiwa kila mara na tembo, viboko na nyati, pia wakiharibu mazao shambani.

"Mwaka huu....nimepata kesi nyingi sana kwenye maeneo hayo ya Stalike. Tembo hawa walifikia mahali wakawa wanakula mazao shambani, pia wameenda kubomoa nyumba za watu kutafuta vyakula na kula vyakula vilivyo ndani ya nyumba za watu," anatamka Diwani, akitaka msaada kiserikali.

"Watuletee kituo cha wanyamapori kwa ajili ya kutusaidia wanyama wanaovuka kutoka hifadhi kuja kijijini, kuwaswaga kurudishwa hifadhini. Sisi tumekuwa tukisaidiwa sana na uongozi wa Hifadhi ya Katavi, lakini utaratibu wao wanawaswaga taratibu wale wanyama kwa kubembeleza kutoka kijijini kwenda hifadhi.

"Sasa ule muda wanawabembeleza wananchi, huku wanaendelea kuumia na sio kazi yao. Hivyo, tunaomba sasa tupatiwe kituo na watu wa maliasili wakae pale Stalike," anasema.

Hapo anaungwa mkono na Diwani Kata ya Mtapenda, Elias Fyula, anayesema:" "Huko nyuma mamba waliua watu wengi sana (eneo la ) Ugala na tulishauri zikatafutwa kampuni zikapewa zabuni ya kuwinda wale wanyama, wakapungua maisha ya watu yakasalimika. Sasa hii hali imeonekana kujirudia...?"



Wanyamapori, simba aliyekula mzoga na mamba katika Hifadhi ya Taifa Katavi. Wamekuwa na athari katika makazi jirani. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

### MWENYEKITI HALMASHAURI

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Nsimbo, Halawa Malendeja, pia Diwani wa Kata ya Ugala, anakiri madhara yakiwamo ya vifo na watu kuliwa na mamba, akitumia mfano mikasa ya kata yake.

"Tunaweza tukawa tunazungumza na kama hakijawahi kukupata unaweza kuchukulia kirahisi tu, lakini likikupata, ndio unaiona changamoto," anafafanua, akitumia mfano wa kata anayoiongoza, wiki kadhaa sasa mwanafunzi wa darasa la saba wa miaka 14 amepoteza maisha.

"Tushukuru wenzetu wa maliasili taarifa zinapotoka wamekuwa wakifika maeneo hayo, sasa wanafika sio kwa maana ya kwenda kuokoa,wanafika tukio limeishatokea, tunaishia sote kusaidiana kulia.

"Kwanini kusiwe na mikakati ya kukomesha hili? Yaani tusipochukua hatua za kuwavuna mamba, tabia ya kuliwa wananchi haiwezi kukoma. Kwa sababu wananchi wa Ugala kwenye ule Mto Ugala ndio sehemu ya kujipatia kipato na ni kawaida kabisa, lakini hii kasi ya watu kuliwa na mamba imekuja hivi karibuni...tunaomba wataalamu watusaidie tupate majibu kitaalamu...

"Nishauri, (watu) wanapofika kule kama wanaenda kuokoa, basi ni vizuri wakawa wanafika na silaha ambazo kweli wataenda kupambana na mamba kuliko ilivyo sasa.

"Juzi tu wameenda kule wakaomba ushirikiano kwa wananchi kwamba huyu mamba, ili tumuue tupeni mbwa au mbuzi tumuue, ili tumtege pale. Mwananchi msamaria akajitokeza akatoa mbwa, alipouliwa akawekwa pale, baadaye wanatoa majibu kuwa 'hata hizi risasi tulizo nazo hazina uwezo wa kuua mamba'. Sasa kama risasi hazina uwezo mlikuja kufanya nini sasa?"anahoji Malendeja.

### HATUA ZA MAZINGIRA

Mwenyekiti wa Kamati ya Mazingira katika halmashuri hiyo, Michael Kasanga, pia Diwani wa Nsimbo, anafafanua: "Tuliomba hili suala la kuvuna mamba liwe la haraka zaidi, kwa sababu tuliweka mikakati kuna umuhimu wa kuwavuna kwa mwongozo wa wataalamu.

"Ilionekana kwamba uvunaji mamba mpaka tupeleke maombi kwenye taasisi ya TAWA, wale ndio watatoa mamlaka ya kuvuna mamba maeneo hayo."

Anasema wameshauri kuharakishwa mradi wa maji kwa maeneo yenye madhara zaidi, kuwanusuru wakazi, kwani mamba huwavizia wanapoenda kuchota maji mtoni.

"Sasa kule kuna shilingi milioni 700 serikali imetenga ili wananchi wa kule wapate maji na mradi upo unaendelea wakati tukiendelea kusubiri kupeleka maombi ya kuvuna mamba tutafute watu ambao wanaweza kuwawinda hao mamba wanaohatarisha maisha ya binadamu."



### DED WA NSIMBO

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Nsimbo, Mohamed Ramadhani, anasema baada ya tukio la mwezi Machi, mtoto kuliwa na Februari, mtu mzima kujeruhiwa, amekagua mkasa na ameandikia barua kwa Wizara ya Maliasili na Utalii, kuomba kibali cha kuvuna, lakini mpaka sasa hawajapewa majibu.

"Sisi kama halmashauri tayari tumeishafikisha matukio yote ambayo yametokea kwa mwaka mzima kwenye eneo hilo ili kuonyesha hatari ya mamba ambao wapo kwenye mto ...bado tunasubiri huo utaratibu ukamilika.

"Wale wanaofuata huduma ya maji...tuombe wale waliopewa tenda, wakamilishe mradi ule haraka iwezekanavyo, ili wananchi waache kufuata maji kule mtoni.

"Hii nayo itasaidia sana, maana wanaathiriwa na mamba wanapokwenda kuchota maji na baadhi yao wakiwa kwenye shughuli za uvuvi," anasema Mkurugenzi Ramadhani.

### OFISA MALIASILI

Ofisa Maliasili wa Halmashauri ya Nsimbo, Jonas Mathias, anasema kutokana na kasi ya matukio yanayoripotiwa kutoka kata Ugala, wameanza kuwasiliana na shirika binafsi linaloitwa Watu na Simba, kusaidia kuripoti uharibifu na madhara ya wanyama.

Anasema, shirika hilo litaegemea vijiji vyote vinavyopakana na Hifadhi ya Taifa Katavi na mto Ugalla, kufanya kampeni za kuelimisha tafsiri ya uharibifu wa wanyama eneo hilo.

Mathias anaeleza, wameanza kuandaa mabango kwenye njia zinazotumiwa kila mara na wananchi kwa safari ya kuchota maji na shughuli zingine za kibinadamu, ili kuwajulisha maeneo hatarishi kwao.

### DC WA TANGANYIKA

Pia, Mkuu wa Wilaya ya Tanganyika, Onesmo Buswelu, anakiambia kikao cha madiwani kuwapo tatizo mahsusi, akitoa mfano wa mkasa wa watu waliopoteza maisha kwa kuumwa na mbwa kichaa.

"Juzi hapa tulikuwa na kichaa cha mbwa kinasumbua. Watu wamepoteza maisha, lakini mwitikio wetu bado nayasema ili tujipime kwamba, wananchi tumewasaidia kiasi gani.

"Mbwa wameuma watu na watoto wengine wamepoteza maisha, lakini bado ofisa anayeshughulika na hilo hatumuoni. Tumekwishatoa maelekezo, aidha mbwa achanjwe au auwawe.

"Hatujui kuwa hili ni janga watu wanapoteza maisha labda mpaka aking'ata watoto wetu au wenzi wetu ndio tuanze kusema kumbe hapa kweli kuna hatari....,"anasema Buswelu.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika, Hamad Mapengo, anatoa ufafanuzi wa tatizo la mbwa lililopatiwa ufumbuzi, kwa wananchi walipatiwa matibabu na hatua zilichukuliwa kuhusu mbwa huyo.

### WAZIRI WA UTALII

Waziri wa Maliasili na Utalii, Mohamed Mchengerwa, akiwa mkoani Katavi kufunga mafunzo ya askari 231 wahitimu mafunzo ya awali, katika Kituo cha Mafunzo ya Jeshi la Uhifadhi, Mlele Mkoani Katavi akatoa maagizo kwa watendaji wa wizara yake.

Maelekezo yake ni kuwatumia askari kutatua tatizo la wanyama wakali wanaovamia makazi ya watu na kusababisha madhara, pia kwa mali.

Anahimiza, utaratibu unaotumika kudhibiti umma kuingia hifadhini, ndio utumike kuzuia wanyamapori kusonga kwenye makazi ya umma, kwa kuwarudisha hifadhini.

MAZINGIRA

KUTOKA NG'AMBO SINGIDA...

# Kutanuliwa huduma maji kulivyojibu kwa mapinduzi zahanati hadi darasani

Na Thobias Mwanakatwe, SINGIDA



Wananchi wa Kijiji Cha Chilejeho Kata ya Chikuyu wilayani Manyoni wakichota maji kwenye bomba ambalo limewekwa katika Shule ya Msingi Chilejeho. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE.**

MWASISI wa taifa wakati huo, Mwalimu Julius Nyerere, alibuni usemi unaobeba maana na ukweli 'maji ni uhai.' Daima katika kipindi chote cha Tanzania huru, suala la maji limebeba kipaumbele.

Bajeti yake kiserikali imekuwa ikiimarishwa kila mwaka , mathalan katika mwaka uliopita 2022/23 Wizara ya Maji ilitengewa matumizi ya Sh. bilioni 709, lakini sasa 2023/24 ni Sh. bilioni 756, ikiwa ni nyongeza ya Sh. bilioni 43.

Manufaa hayo na mikakati tangu zamani, tafsiri yake inaangukia mkoani Singida, sasa wakijinasibu asilimia 64 ya maeneo vijijini, kunapata maji safi na salama, matarajio katika bajeti hiyo inayoishia ukingoni 2022/23, huduma itafika asilimia 68 kimkoa.

Matunda yake yakoje? Uongozi wa elimu mkoa wa Singida unajisifu tangu umefikishiwa huduma ya maji, kiwango cha mahudhurio darasani na ufaulu umeongezeka maradufu, ikilinganishwa na awali.

Vilevile, kunaelezwa kiasi cha maambukizi ya magonjwa kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine inakabiliwa, kwa mfano wa zahanati 36 zilizopo wilayani Manyoni, 20 zina huduma ya maji safi na salama.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya Manyoni, Dk.Furaha Mwakafwila, anasema utoaji huduma za afya kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali, umekuwa rahisi kutokana na kupatikana huduma ya maji.

Meneja wa Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira (RUWASA) Wilaya ya Manyoni, Mhandisi Gabriel Ngongi, anasema hali ya upatikanaji maji katika wilaya hiyo, vijijini kwa sasa imefikia asilimia 55.

Anaungwa mkono na Ofisa Elimu Sekondari Wilaya ya Manyoni, Adeline Mwanisi, anayesema kati ya shule 21 za serikali wilayani humo, 10 zimeshafikishiwa huduma ya maji na sita kazi ya kuziunganishia zinaendelea, aki

zitaja ni: Mhalala, Manyoni, Mwanzi, Makulu, Chikuyu, Nkonko, Iseke, Sanza na Saranda.

Mwanisi anasema tangu kuunganishwa maji, kiwango cha mahudhurio ya wanafunzi darasani na ufaulu umeongezeka, ikilinganishwa na awali, utoro ulikuwa juu kwa sababu wanafunzi walitumia muda mrefu kufuata maji mbali kwa ajili ya matumizi shuleni.

Anasema, pia maji yamerahisisha kazi ya kujenga madarasa na vyoo vya wanafunzi vimekuwa visafi, huku wanafunzi nao wamebaki nadhifu muda wote.

Baadhi ya wasichana wanaosoma, wanatamka wengi walikuwa hawahudhurii masomo siku za hedhi, kwa sababu ya uhaba wa maji shuleni, lakini hivi sasa kizuizi hicho kimetoweka.

"Kati ya siku nne ninazotumia kwenye siku zangu, siku tatu huwa nashindwa kuja kabisa shuleni, hata nikibeba dumu la maji, bado huwa hakiwezi kukidhi mahitaji yangu yote, tunaomba tuchimbiwe visima," anatamka mwanafunzi wa Shule ya Chilejeho, wilayani Manyoni.

Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) mkoa wa Singida, Lucas Said anasema: "RUWASA ilipoanza Julai 2019, hali ya upatikanaji maji katika Mkoa wa Singida ilikuwa asilimia 49.5, lakini hadi kufikia Machi 2023 imefikia asilimia 64, hivyo tuna uhakika wa kufikia malengo ya asilimia 85 kutokana na serikali kutupatia mtambo wa kuchimbia visima."

Saidi anasema, mtambo huo umepokewa Singida Februari mwaka huu na sasa umeshachimba visima zaidi ya vitano, ikiwamo Singida Vijijini visima sita, wilayani Ikungi visima vinne na sasa unatumika wilaya ya Manyoni, kunakochimbwa visima vitano, lengo ni kila wilaya kuchimbwe visima.

Dk. Mwafwila anafafanua: "Katika Sekta ya Afya inapendeza kujenga vyoo ambavyo ni vya kuflashi. Pia, kuwapo maji nako kumesaidia kupunguza magonjwa yanayosababishwa na maji, mfano magonjwa ya kuhara, taifodi na trakoma ambao siku hizi hausikiki kabisa, kwa sababu watu wananawa uso vizuri."

Anasema upatikanaji maji, pia umesaidia kukabili kipindi cha homa ya Uviko 19, wananchi wengi wakazingatia watumia maji, sasa wamedhibiti kipindupindu mkoani kwa miaka kadhaa, mchango mkubwa ni wa maji.

**SAUTI YA RUWASA**

Meneja wa RUWASA wilaya ya Manyoni, Mhandisi Gabriel Ngongi, anasema miradi kadhaa ya maji inayoendelea kujengwa wilayani hapa inafika asilimia 80, kukitarajiwa itakamilika mwaka wa fedha uliopo, unaoisha Juni 30 mwaka huu.

Mhandisi Ngongi anaitaja miradi hiyo ya maji inayoendelea kujengwa ni wa Njilii, utakaohudumia takribani wastani watu 3,000, mradi wa maji kijiji cha Mabondeni, utakaohudumia watu 2, 500; Rift Valley utakaowahudumia vijiji vinne; na mradi wa maji wa Kintinku-Lusilile, utakaohudumia vijiji 11 vyenye wakazi 55,000.

Anasema upatikanaji maji umeisaidia sekta ya elimu, kwa wanafunzi kutumia muda mrefu kusoma, tofauti na awali walitumia kutafuta maji.

Meneja huyo wa RUWASA, anasema pia upatikanaji maji umewasaidia wananchi kuepuka magonjwa yanayosababishwa na ukosefu wa maji.

Meneja wa RUWASA, Mazingira Vijijini mkoa wa Singida, Lucas Said, anasema wakati wa kujenga miradi ya maji, wamekuwa wakihakikisha kila taasisi zilizopo eneo husika, kama shule za msingi na sekondari, chuo, zahanati,vituo vya afya na hospitali zinapatiwa huduma ya maji, kwa kuwa ni maeneo ya kimkakati.

Saidi anasema, hadi sasa RUWASA imepanga kutumia Sh. bilioni 15.6 kwa ajili ya kutekeleza miradi 37 ya maji katika mwaka wa fedha ujao, unaoanza Juma Mosi, mkakati ni kupunguza kero ya maji mkoani humo.

Anasema, miradi hiyo itakayojengwa katika mwaka wa fedha ujao itaongeza upatikanaji maji vijijini mkoani hapa, kutoka asilimia 68 hadi asilimia 78.

"Hadi kufika Juni 2025 kwa mikakati ambayo RUWASA tumejiwekea kiwango cha upatikanaji maji kitafika asilimia 86, ambayo ni zaidi ya lengo la asilimia 85 lililowekwa," anasema.

Kwa mujibu wa ofisa huyo wa RUWASA, katika mwaka unaoisha wa fedha, Singida ilipokea Sh. Bilioni 11 kutoka Mfuko wa Taifa wa Maji na Mfuko wa Malipo kwa Matokeo kwa ujenzi wa miradi ya maji mkoani humo.

# UTALII TIBA ALIYOWEKEZA RAIS 2021, ZAO LAKE MABINGWA WATIBU 500 MALAWI

Inatoka Uk. 11

ma

**MATUNDA YALIVYO**

Hivi karibuni, kamati hiyo imeandaa safari ya madaktari bingwa watano kwenda Malawi, hata wakafanikiwa kuwahudumia wagonjwa 724 kwenye kambi ya wiki moja iliyofanyika kwenye Hospitali ya Queen Elizabeth, jijini Blantyre, Malawi.

Waziri wa Afya nchini Malawi, Khumbize Chiponda, anasema Malawi na Tanzania wamekubaliana kushirikiana katika kujengeana uwezo, kwani nchi hiyo haijaweza kuanzisha hospitali ya moyo, akisema ni ya gharama kubwea kuianzisha. Hadi sasa Malawi inatajwa kuwa na wagonjwa zaidi ya 500.

**USHUHUDA WA MABINGWA**

Madaktari hao waliporejea nchini, wakatoa ushuhuda mzito waliyoyafanya Malawi, kiongozi wa msafara, daktari bingwa wa maradhi ya Moyo wa JKCI, Dk. Angela Muhyoza, anasema walikuwa na madaktari bingwa wa watoto wawili na mabingwa wa watu wazima wawili na wataalamu wengine waliowasaidia.

Anafafanua, kati ya wagonjwa waliowahudumia, 524 waligundulika na matatizo ya moyo, baadhi yao walipatiwa tiba na wagonjwa 200 walihitaji huduma za upasuaji mkubwa wa kufungua kifua.

"Miongoni mwa wagonjwa hao, 60 wanahitaji matibabu ya haraka kutokana na matatizo waliyo nayo kwa hiyo wasipopata matibabu ndani ya muda huo wanaweza kupata matatizo zaidi, wananchi wa Malawi wamefurahia huduma zetu na walitamani tuendelee kuwepo nchini kwao," alisema

Daktari bingwa wa magonjwa ya moyo kwa watoto kutoka JKCI, Parvina Kazaura, anasema katika kambi hiyo, walifanya uchunguzi na matibabu ya moyo kwa watu wazima na watoto.

Anasema, kila siku walitibu watoto zaidi ya 80, akifafanua: "Kwa bahati mbaya watoto wengi wenye magonjwa ya moyo ya kuzaliwa nayo, wamekuja wakiwa na umri mkubwa, ambao walipaswa kufanyiwa upasuaji mapema baada ya kuzaliwa lakini hawakufanyiwa kutokana na huduma hizi kutokuwapo Malawi."

Dk. Parvina anasema wamewashauri wataalamu wa afya wanaowahudumia, dawa gani wanazopaswa kuzitumia kuwatibu.

Mkuu wa Idara ya Magonjwa ya Ndani kutoka Hospitali ya Queen Elizabeth, Malawi Dk. Chimota Phiri, anaisema kambi ya wenzao kutoka JKCI imewapa mwanga kuyatambua magonjwa ya moyo waliyo nayo wananchi wa Malawi

**KUTOKA WIZARANI**

Mkurugenzi wa Magonjwa ya Nje Wizara ya Afya, Dk. Asha Mahita, anapongeza kazi kubwa ya Kamati ya Kitaifa ya Utalii Tiba tangu wateuliwe. Anasema, imechukua muda mrefu dhana ya utalii wa tiba kufahamika hasa kwenye hospitali za hapa nchini, akisema utasaidia kiwango kikubwa kuongeza mapato ya serikali kwa wageni watakaokuja.

Anasema pamoja na kuongeza mapato kutokana na utalii wa tiba hata watu binafsi watakuwa wakinufaika kwa kuleta wagonjwa kutoka mataifa mbalimbali na hospitali husika itakayopokea wagonjwa hao itanufaika.

MAZINGIRA

# Mbunge na staili ya ofa, maji bure kwa wapigakura, wiki mara mbili



Baadhi ya wakazi wa Mtaa wa Bukondamoyo, Kata ya Mhungula Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, wakiwa katika mstari wa kuchota maji yanayogharamikiwa na Mbunge wa Kahama, Jumanne Kishimba. **PICHA: SHABAN NJIA**

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

RIPOTI ya Wakala wa Usambazaji wa Maji Vijijini (RUWASA) wilayani Kahama, mkoa wa Shinyanga katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, inatamka kukamilisha miradi 652 ikiwa na vituo vya kuchota maji 11,457 ambayo inahudumia vijiji 1,052 na kunufaisha wananchi wapatao 3,824,914.

Jumanne Kishimba, Mbunge wa Jimbo Kahama kutoa mchango wake kusaidia, ameibua utaratibu wake, kwa wananchi wanaoishi pembezoni mwa mji na hawajapata mtandao wa maji, wauchote maji bure kila siku ya Jumanne ya Ijumaa, lengo ni kuwaondolea adha ya kukosa maji.

Anasema, wananchi wanaoishi pembezoni akidai wamesahaulika, hivyo ameona kuwajali na kuwasogeza huduma ya maji safi na salama bure kupitia maghati ya maji yaliyojengwa au kumilikiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama (KUWASA) na yeye kulipia bili baada ya matumizi.

Anasema, ofa hiyo inatolewa kwa wakazi wa kata za Mhungula, Nyahanga na Nyihogo Manispaa ya Kahama, kwani ni maeneo yamekuwa na changamoto ya upatikanaji maji ya uhakika, wakinunua ndoo ya lita 20 na lita 10 kwa Sh.50 na wale wasiokuwa na uwezo kutumia maji machafu.

Kishimba anasema, kisheria serikali ilipaswa kutoa huduma hiyo ya maji bure, akisema baadhi wanatumia maji machafu na wanyama wanaowafuga, sasa anawatatulia kwa kutoa ofa ya kuchota bure kwa siku hizi mbili za wiki.

Anasisitiza, uchotaji huo bure ni endelevu na litakoma hadi siku wananchi wakipata maji kwenye makazi yao na kuwataka wale wenye mtandao wa maji katika makazi yao kuwapatia kipaumbele wasiokuwa na maji ili kuepusha migogoro ambayo isiyokuwa na tija kwani huduma hiyo haijali unamaji ndani au laah.

> **"Sasa tunaondokana na kutumia maji machafu, kuchangia na mifugo tunayofunga na kumuomba kuongeza siku nyingine ya Jumamosi ili wanafunzi nao wapate muda wa kufanyausafi wa mavazi yao?"**

**WANUFAIKA WA OFA**

Mnufaika Ashura Omary, mkazi wa mtaa wa Bukonyamo, anasema kabla ya kupewa ofa hiyo, alikuwa wakitumia maji ya kwenye visima walivyochimba wao na wakati mwingine kulazimika kuomba maji kwa baadhi yao wenye huduma hiyo majumbani kwa kuchangia bili mwisho wa mwezi.

Anasema, mtaani kwao kuna gati la maji ambalo wanachota maji kwa Sh.50 kwa ndoo ya lita 20 na lita 10, kwa wale wasiokuwa na uwezo wa kumudu gharama hizo wanalazimika kutumia maji ambayo sio safi na salama na anamshukuru mbunge kwa kuliona hilo na kuchukua hatua ya kutenga siku ya Jumanne ya kuchota maji bure.

Mwingine Jenipha William, wa Mtaa wa Shunu, anasema changamoto iliyopo, ni kwa wenye mtandao wa maji majumbani, nao wanatumia maji hayo siku ya Jumanne, hali inayowafanya kupata bili ndogo za kila mwezi na anawasihi kuwapatia kipaumbele wale wasiokuwa na huduma hiyo katika makazi yao ili kunufaika na ofa ya mbunge wao.

"Tunaoishi pembezoni mwa mji ambapo huduma ya majisafi na salama haijafika tunapata tabu sana, kwanza tunatumia maji ya kwenye visima ambayo tumevichimba wenyewe kando ya makazi yetu na wataalamu wanadai vinaingiliana na vyoo tunavyotumia chini kwa chini na hatuna namna tunatumia tu tunapoumwa maradhi tunajitibia," anasema William.

Anaongeza kuwa: "Hawana budi kumshukuru Mbunge Kishimba kwa kuliona tatizo hilo na kutenga siku ya Jumanne ya kila wiki ya kuchota maji bure na yeye kutulipia bili.

"Sasa tunaondokana na kutumia maji machafu, kuchangia na mifugo tunayofunga na kumuomba kuongeza siku nyingine ya Jumamosi ili wanafunzi nao wapate muda wa kufanyausafi wa mavazi yao?"

**KUTOKA KUWASA**

Eva Emannuel, msimamizi wa ghati la maji Mtaa wa Bukondamoyo, anazungumza kwa niaba ya wasimamizi wa maghati, akisema, siku hiyo ya ofa wateja huwa wengi kulinganisha na siku za kulipia huduma kwa Sh.50 kwa kila ndoo ya lita 20 na lita 10 na mwisho wa siku hiyo bili huwa ni kubwa na inalipwa na mbunge tena kwa wakati bila usumbufu.

Anasema, kwa siku za kawaida huwa wanatoa huduma kuanzia asubuhi saa moja hadi saa sita anafunga na baadaye kufunga saa tisa alasili hadi saa kumi na mbili jioni na wateja huwa wachache, lakini siku ya ofaa huwa bomba linakuwa wazi siku nzima, kazi inayoendelea ni kuhesabu 'uniti' za maji zilizotumika na kuziwasilisha kwenye ofisi ya mbunge, kwa ajili ya malipo.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Kahama (KUWASA), Mhandisi Alen Marwa, anasifu mbunge kuhakikisha wananchi wanaoishi pembezoni mwa mji wanapata huduma ya majisafi na salama kwa kuwakinga na maradhi.

Mhandisi Marwa anasema, Manispaa ya Kahama inajumla ya kata 20 na kuna baadhi ya kata mtandao wa majisafi na salama haujawafikia wananchi kwa asilimia kubwa hasa zile za pembeni ambazo wanashirikiana na Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini(RUWASA) kuhakikisha zinapata maji na kuepuka kutumia maji na wanyama.



# H'shauri zaagizwa kutenga fedha usafiri wa dharura

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

HALMASHAURI zimeagizwa kuhakikisha gharama za usafiri wa dharura kwa wajawazito na watoto wachanga wazijumuishe kwenye mipango na bajeti zao.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Deogratius Ndejembi alitoa agizo hilo jijini hapa alipokuwa akifungua kikao kazi na kugawa vitendea kazi kwa waratibu wanaosimamia mfumo wa usafirishaji wa dharura kwa wajawazito, waliojifungua na watoto wachanga (M-mama).

Ndejembi alisema hatua ya kuweka huduma hiyo kwenye mipango ya kila halmashauri kutasaidia kuimarisha na kuifanya huduma ya dharura kwa wajawazito, wanaojifungua na watoto wachanga katika halmashauri kuwa endelevu.

"Serikali imeleta mfumo huu ili kutatua matatizo ya rufaa na usafiri wa dharura kwa wajawazito, waliojifungua na watoto hapa nchini. Bado tuna tatizo kubwa kwenye usafiri wa dharura, na jambo hili ni moja ya vipaumbele katika kuokoa maisha ya wajawazito na watoto wachanga wanapokuwa na dharura za kiafya na ndiyo maana imekuja na mfumo huu,"alisema.

Alihimiza ushirikiano kwa wadau wote wanaohusika katika kuutekeleza mfumo wa M-mama na kuhakikisha gharama za usafiri wa dharura zimejumuishwa katika mipango na bajeti kwa kila halmashauri.

Mkuu wa TEHAMA kutoka Wizara ya Afya Zanzibar, Mahamed Mafazy alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar utekelezaji wa mfumo huo ulianza Desemba 20 mwaka jana, wameshahuduma wajawazito 778.

Alisema kwa sasa imejipanga kuufanya mfumo huo kuwa endelevu kwa kuanzisha mfuko ambao utamlazimisha mwananchi kuwa na bima ya afya na kuifanya huduma ya magari ya wagonjwa kufanywa na sekta binafsi, huku mfumo wa M-mama ukipewa kipaumbele.

Meneja wa Vodacom Tanzania Kanda ya Kati, Joseph Sayi alisema katika kutekeleza mfumo huo mpaka sasa safari 21,000 zimefanyika na kuokoa maisha ya watoto wachanga na kinamama zaidi ya 805.

Alisema ili kufanikisha usambazaji mfumo huo, Vodacom Tanzania imetoa Dola za Marekani milioni 10 na Shirika la USAID limetoa Dola za Marekani milioni tano.

**Kufanikisha usambazaji mfumo huo, Vodacom Tanzania imetoa Dola za Marekani milioni 10 na Shirika la USAID limetoa Dola za Marekani milioni tano.**

# Maofisa biashara watakiwa kuainisha kero za w'biashara

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara imewataka maofisa biashara ngazi za mikoa na halmashauri hapa nchini kuainisha kero zinazowakabili wafanyabiashara katika maeneo yao na kuzitafutia ufumbuzi.

Kaimu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Conrad Milinga aliyasema hayo jana wakati akizungumza na maofisa biashara wa mikoa kikao kilichohusu kuipitia rasimu ya mwongozo wa kuboresha mazingira ya biashara ngazi za mikoa.

Alisema nia ya serikali ni kuweka mazingira wezeshi kwa wafanyabiashara kuanzia ngazi za chini.

"Tunahitaji kupata taarifa kila mwezi ya hali ya bei ya bidhaa na hizi taarifa tunategemea kupata kutoka kwenu, tuweke mfuko fulani wa taarifa tutakazopata kutoka kwenu tunavyoongea huko juu ndiyo tunachokiongea huku chini, tusitofautiane."

"Tunataka mapato hivyo ni lazima tutengeneze watu ambao watatupa mapato. Suala la kuamka asubuhi unakwenda kufunga biashara ya mtu hapama, tunataka tumjengee uwezo aone ana wajibu gani kwa serikali. Lisiwe suala la kusukumana, mtusaidie kutoa elimu ili aone ofisa biashara ni msaada," alisema.

**Wawekezaji wanaokuja ambao wanaitwa na Rais Samia hawawekezi hewani wanawekeza kwenye mikoa na halmashauri, hivyo tusipofanya vizuri tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu.**

Aidha, alisema wataalamu hao wataangalia mpango wa kuboresha mazingira ya biashara ikiwamo kuangalia ukuaji wa sekta binafsi.

"Uwekezaji unaofanyika huko kwenye ngazi za mikoa na halmashauri ufikie malengo yaliyowekwa, sisi kama serikali ina majukumu yake inawezekana bado tuna mawazo yale ya zamani tunapoiona sekta binafsi bado tunaitazama kwa mtazamo hasi."

"Sisi watendaji wa serikali tunaanza kupambana na sekta binafsi kama ni washindani badala ya kuiona yenyewe inasaidia jitihada zinazofanywa na serikali,"alisema.

Alisema maofisa hao ni wasimamizi kwenye mikoa na halmashauri kuhusu sheria, sera, kanuni na taratibu.

"Wawekezaji wanaokuja ambao wanaitwa na Rais Samia hawawekezi hewani wanawekeza kwenye mikoa na halmashauri, hivyo tusipofanya vizuri tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu," alisema.

Alisema taasisi simamizi za masuala ya biashara zipo kwenye wizara hiyo, hivyo maofisa hao wanasaidia kutekeleza majukumu kwa niaba yao.

"Tunaandaa mwongozo wa kuwawezesha wafanyabiashara, wajasiriamali wajue wanapotaka kuanzisha biashara waanzie wapi na aiishie wapi, kuna njia zipi anapaswa kufuata na watekelezaji wa mwongozo ni ninyi,"alisema.

Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Biashara wa wizara hiyo, Sempeho Manongi, alisema kikao hicho kitafanyika kwa siku mbili na kitalenga kuwapa uelewa wa majukumu yao, mpango wa kuboresha mazingira ya biashara na kupitia mwongozo huo ili kuufanyia maboresho.



Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, akizungumza na wakazi wa mtaa wa Ndachi, Kata ya Mnadani jijini humo juzi, alipokuwa akijibu malalamiko yanayohusiana na migogoro ya ardhi inayowakabili. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wakuu wa shule watakiwa kuacha ubosi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

KATIBU Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Fatma Mganga, amewataka maofisa elimu na wakuu wa shule kuacha 'ubosi' badala yake wafanye kazi kwa bidi.

Pia amewataka kufanya tathmini kujua matatizo ambayo yanarudisha nyuma kiwango cha elimu mkoani hapa.

Akizungumza jana wakati wa mkutano uliowashirikisha wakuu wa shule, maofisa elimu ngazi ya mkoa, wilaya, kata wenye lengo la kufanya tathmini ya matokeo ya mitihani ya kitaifa ya darasa la nne na saba.

Dk. Mganga alisema maafisa elimu na wakuu wa shule watumie mbinu mbalimbali kusimamia taaluma ili kuhakikisha ufaulu unaongezeka katika shule za msingi.

Alisema maofisa elimu wanapaswa kuwa watatuzi wa kero za walimu, kuzitembelea shule na kuja na mikakati ya kuboresha elimu na kila mwalimu anatimiza majukumu yake na kufanya kazi kwa ushindani.

Dk.Mganga alisema wakuu wa shule wanapaswa kufanya tathimini kila wiki kwa walimu na masomo wanayofundisha ili kubaini mapungufu na namna ya kutatua kufanya hivyo kusaidia kuwapima kutokana na matokeo.

Dk. Mganga aliongeza kuwa watendaji wengine na maofisa elimu watoke maofisi kwenda kwenye shule ambazo zinamatatizo na kufanya tathmini ya wanafunzi ambao wanashindwa kuwa na matokeo mazuri.

"Kiongozi unaweka mikakati ili kuweza kupata matokeo usisikilize 'rumors' (uvumi) tumia jitihada zako upate matokeo ili uweke 'legacy', (alama)" alisema.

Alisema viongozi mkoani hapa wanapaswa kufanya kazi kwa kujituma ili waweze kuweka alama, hivyo akasisitiza walimu wakuu kujituma na kujitoa zaidi kwenye kutoa elimu kwa wanafunzi.

Mratibu wa Programu ya Serikali ya Shule Bora Mkoa wa Singida, Samweli Daniel, aliwashauri wadau wa elimu wanapopanga mipango ya kuboresha elimu iwe inaandikiwa ripoti ili zitumike wakati wa utekelezaji katika maeneo mbalimbali.





# H/shauri zaagizwa kutekeleza miradi ya faida kiuchumi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HALMASHAURI nchini zimeshauriwa kuanza kutekeleza miradi yenye faida kiuchumi kwa kutumia mfumo wa ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP) ili kuharakisha utekelezaji wa miradi hiyo na kuanza kupata faida mapema.

Kamishna wa Ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi nchini, David Kafulila alitoa ushauri huo jijini Mbeya alipokuwa anafungua mafunzo ya ubia kwa baadhi ya watendaji wa halmashauri za Mkoa wa Mbeya.

Mafunzo hayo yaliwashirikisha wakurugenzi wa halmashauri, wachumi, maofisa manunuzi, wahandisi pamoja na maofisa kutoka katika taasisi mbalimbali za kifedha.

Kafulila alisema miradi mingi ya halmashauri huwa inachelewa kukamilika kutokana na kutengewa bajeti huku watendaji wakitegemea fedha kutoka hazina jambo ambalo linasababisha baadhi kutotekelezwa kabisa.

Alisema miradi mingi ya halmashauri inayotegemea fedha kutoka hazina huwa inakataliwa kutokana na ufinyu wa bajeti na hivyo njia pekee ya kuharakisha miradi hiyo ni kuwashirikisha wadau ili baadhi itekelezwe kwa ubia.

**Mfumo wa PPP unafanya kazi duniani kote na ni mzuri kwa sababu unaharakisha miradi, miradi ambayo inaweza ikatekelezwa kwa njia kama hii ni masoko, vituo vya mabasi na miradi mingine yenye faida.**

"Mfumo wa PPP unafanya kazi duniani kote na ni mzuri kwa sababu unaharakisha miradi, miradi ambayo inaweza ikatekelezwa kwa njia kama hii ni masoko, vituo vya mabasi na miradi mingine yenye faida," alisema Kafulila.

Alizitaka taasisi za fedha nchini kushiriki kutoa elimu kwa wadau kuhusu faida za kutekeleza miradi kwa kutumia mfumo wa PPP huku akizitaka pia kushiriki kwenye utekelezaji wa miradi hiyo.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo walisema mfumo huo ni mzuri kwenye utekelezaji wa miradi kwa maelezo kuwa unaharakisha miradi kukamilika.

Kaimu Mchumi wa Jiji la Mbeya, Cosmas Kyovecho, alisema wakitekeleza miradi kwa mfumo huo ni rahisi kupata fedha na hivyo kutekeleza miradi mingi kwa wakati mmoja na faida ikaanza kupatikana mapema.

Alisema miradi inayotekelezwa kwa kutumia fedha kutoka hazina pekee huwa inachelewa kukamilika na hivyo tija yake kuchelewa pia kuanza kuonekana.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Stephene Katemba, alisema baada ya mafunzo hayo alibaini kuwa katika halmashauri yake kuna fursa kubwa ya kutekeleza miradi kwa mfumo huo wa PPP.

Alisema eneo ambalo linafaa kutumia mfumo huo ni uwekezaji katika ardhi hasa upimaji wa maeneo na ujenzi wa baadhi ya miradi ikiwamo maghala, masoko na hata nyumba za kuishi.

Mshauri wa Sera za Uchumi, Bajeti na Kodi kutoka Wizara ya Fedha, Prof. Handleya Mafwenga, alisema awali serikali haikuwa na sera nzuri kuhusu masuala ya ubia na kwamba ndiyo sababu ushiriki wa sekta binafsi ulikuwa mdogo.

Alisema kwa sasa sera zimeboreshwa na zinawavutia wadau mbalimbali kushirikiana na serikali kwenye utekelezaji wa miradi hasa ile inayoonekana kuwa na faida kiuchumi.




Meneja wa Benki ya Afrika Tanzania, tawi la Mbeya, Agatha Lyimo (kulia), akikabidhi zawadi ya simu janja kwa Victor Thomas Sowani, aliyeibuka mshindi wa droo ya kwanza ya promosheni ya benki hiyo ya kuhamasisha matumizi ya simu kupata huduma za kibenki inayojulikana kama "Fanya Muamala na Ushinde" iliyofanyika katika tawi hilo, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jiji Mbeya latoa mil.15/- ujenzi vyoo shule ya sekondari

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya, imetoa Sh. milioni 15 kwa ajili ya ujenzi wa vyoo vyenye matundu 20 katika Shule ya Sekondari Kalobe baada ya vilivyokuwa vinatumika awali kubomoka.

Meya wa Jiji hilo, Dor-Mohamed Issa, aliyasema hayo juzi alipofanya ziara katika shule hiyo kwa lengo la kuangalia maendeleo ya mradi huo ambapo aliwataka wasimamizi wa mradi huo kuhakikisha wanautekeleza vizuri.

Alisema serikali imetoa fedha hizo ili kuwasaidia wanafunzi wa shule hiyo ambao wamekuwa wakihangaika baada ya vyoo vya awali kubomoka na kwamba yeyote atakayezitumia vibaya atashughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

Alisema mradi huo kwa sasa umefikia hatua ya kuezekwa na hivyo wanakusudia kupeleka fedha zingine kwa ajili ya kukamilisha ili vianze kutumika mapema.

"Nimeridhika na kasi ya ujenzi wa vyoo hivi ambavyo ni vya watoto wetu wa kike, lakini nitoe angalizo kwa wasimamizi wasije wakacheza na fedha hizi, hapa tunategemea kuleta zingine kwa ajili ya umaliziaji na lazima zitumike kwa lengo hilo," alisema DorMohamed.

Alisema serikali inaboresha mazingira ya elimu kwa lengo la kuinua kiwango cha elimu nchini na hivyo akawataka viongozi wa serikali walioko kwenye ngazi ya kata na mitaa kusimamia vizuri.

# Mkuu wa mkoa awapa siri ya utajiri wakazi Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI mkoani Mbeya wameshauriwa kuchangamkia fursa ya ufugaji nyuki kwenye maeneo ili kujiongezea kipato kwa kuuza mazao mbalimbali ya nyuki ambayo soko lake limekuwa likiongezeka kwa kasi duniani.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alitoa ushauri huo juzi alipozindua maadhimisho ya Siku ya Nyuki Duniani ambayo kimkoa yalifanyika katika Kata ya Itewe Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Homera alisema ufugaji wa nyuki mbali na kuwa chanzo cha mapato lakini pia ni moja kati ya njia zinazosaidia kwenye uhifadhi wa mazingira na hivyo wananchi wanatakiwa kushiriki ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Alisema serikali kupitia Ofisi ya Rais, Muungano na Mazingira imekuwa ikifanya juhudi mbalimbali za kutunza mazingira na hivyo wananchi wanatakiwa kuipokea miradi inayoanzishwa kwa ajili ya faida yao wenyewe.

Alisema asali inayotokana na nyuki ni lishe na ni dawa ambayo inasaidia kukabiliana na magonjwa mbalimbali na hivyo akawataka wananchi kuitumia ili kuimarisha afya zao.

Homera alisema katika mkoa huo kuna maeneo mbalimbali ambako mradi wa urejeshaji endelevu wa mazingira na hifadhi ya bioanuai kwa lengo la kurejesha rutuba kwenye baadhi ya maeneo ambayo yameharibiwa.

Vilevile alisema lengo la mradi huo ni urejeshaji wa ardhi iliyoharibiwa na uhimilivu wa mifumo ya ikolojia, hivyo akawataka wananchi kuutekeleza kwa kuzingatia maelekezo na miongozo wanayopewa ili wafaidike.

Ofisa Nyuki wa Mkoa wa Mbeya, Marietha Kereti, alisema Mkoa wa Mbeya una wafugaji binafsi wa nyuki 527 na vikundi vya wafugaji 159 ambavyo vipo katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo.

Alisema kwa mujibu wa sensa waliyoifanya mkoa huo una mizinga ya asili 63,608 na mizinga ya kisasa ipo 16,153 na kwamba mizinga mingi ipo katika halmashauri za Chunya, Mbeya, Mbarali na Rungwe.

Alisema mwaka wa fedha 2021/2021 uzalishaji wa asali katika mkoa huo ilikuwa tani 682.43 ambayo ilikuwa na thamani ya zaidi ya Sh. bilioni tano na nta iliyozalishwa ilikuwa tani 1.6 ambayo thamani yake ilikuwa Sh. milioni 9.8.

Alisema ufugaji wa nyuki pia unasaidia kwenye uchavushaji wa mimea na hivyo kusaidia pia kwenye uendelezaji wa bioanuai na utunzaji wa mazingira.

Baadhi ya wafugaji wa nyuki walioshiriki maadhimisho hayo waliiomba serikali iwasaidie kuboresha miundombinu ya barabara katika maeneo yao ili iwarahisishie usafirishaji wa mazao yao.

Mmoja wa wananchi hao, Julius Zacharia ambaye ni mkazi wa Kijiji cha Tembela alisema ufugaji wa nyuki ni shughuli ambayo haihitaji gharama kubwa kama ilivyo kwenye kilimo.



## Serikali yakiri Bandari ya Malindi Unguja kuelemewa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Nadir Abdulatif Yussuf amekiri kuwapo kwa msongamano wa abiria katika Bandari ya Malindi Unguja, kwamba serikali imeanza mikakati ya kuimarisha Bandari ya Mkokotoni ili kumaliza tatizo hilo.

Aliyasema hayo wakati akijibu swali la mwakilishi wa Viti Maalumu, Fatuma Ramadhan Mandoba aliyetaka kujua juhudi zinazochukuliwa na wizara kupunguza msongamano wa abiria katika Bandari ya Malindi kwa sasa.

Alisema wizara imeanza kuchukua juhudi katika kukabiliana na matatizo ya matumizi ya Bandari ya Malindi ambayo ni kubwa na inatoa huduma za abiria pamoja na mizigo.

Alisema tayari wizara imetenga eneo la Maruhubi Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja kwa ajili ya kushusha na kuweka makontena yote yanayoshushwa kutoka katika meli za mizigo.

Alisema tayari eneo hilo limeanza kupokea makontena hayo ambapo kwa kiasi kikubwa limepunguza msongamano wa makontena na mizigo katika Bandari ya Malindi.

Aidha, alizitaja mikakati mingine zinazotarajiwa kuchukuliwa ni pamoja na kuimarisha Bandari ya Mkokotoni iliopo Mkoa wa Kaskazini Unguja ambayo itatumiwa na abiria wanaotoka katika Kisiwa cha Pemba.

Alisema wizara yake inaendelea na mchakato wa kutafuta wawekezaji kwa ajili ya ujenzi wa bandari shirikishi eneo la Mangapwani Mkoa wa Kaskazini Unguja ambayo itakuwa na uwezo mkubwa wa kutoa huduma za aina mbalimbali.

**Tayari eneo hilo limeanza kupokea makontena hayo ambapo kwa kiasi kikubwa limepunguza msongamano wa makontena na mizigo katika Bandari ya Malindi.**

# Kamati yaagiza ongezeko kasi utoaji mikopo wajasiriamali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMATI ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi imeitaka Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kuongeza kasi ya utoaji mikopo kwa wajasiriamali na wafanyabiashara ili kwenda na dhamira na malengo ya serikali ya kuwakomboa wananchi kiuchumi.

Hayo yalisemwa jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi Chukwani na Mwenyekiti wa kamati hiyo, Sabiha Filfil Thani wakati akiwasilisha maoni ya kamati hiyo katika bajeti ya Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji.

Alisema kasi ya utoaji wa fedha za mikopo kwa wajasiriamali wadogo ni ndogo.

Alisema serikali imetenga Sh. bilioni 29.3 kwa ajili ya wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo kuchukua mikopo nafuu na kufanya shughuli zao za uzalishaji mali hatua ambayo imelenga kuwakomboa kiuchumi.

"Mheshimiwa Spika serikali imetenga fedha nyingi kwa wajasiriamali wadogo ikiwamo wafanyabiashara lakini bado lipo tatizo la urasimu wa utoaji wa fedha hizo hali inayowakatisha tamaa wahusika," alisema.

Pia aliipongeza Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) kwa kufanya kazi na kuongeza kasi ya uwekezaji kwa kuiboresha taasisi hiyo kuwa ya kupigiwa mfano na bora zaidi katika bara la Afrika kwa kukamilisha taratibu za uwekezaji katika kipindi kifupi.

Aidha alisema ZIPA imefanikiwa kusajili miradi ya uwekezaji 74 ya Sh.trilioni 105 ikiwemo ukodishwaji wa visiwa vidogo 16 viliopo Unguja na Pemba.

**ZIPA imefanikiwa kusajili miradi ya uwekezaji 74 ya Sh.trilioni 105 ikiwemo ukodishwaji wa visiwa vidogo 16 viliopo Unguja na Pemba.**

Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia makadirio mapato na matumizi ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Kazi na Uwezeshaji wametaka kuwepo kwa kasi ya utoaji wa mikopo kwa wajasiriamali wadogo kwa sababu fedha zipo.

Mwakilishi wa Mfenesini, Machano Othman Said, aliipongeza ZIPA kwa kufanya kazi kubwa ya maboresho yake hatua ambayo imesaidia kuwepo kwa kasi ya uwekezaji huku mazingira yakiimarishwa.

Baraza la Wawakilishi lilipitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2023-2024 Sh.bilioni 8.2 kwa kazi za kawaida na maendeleo.




Waziri wa Fedha na Mipango Zanzibar, Dk. Saada Mkuya akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani nje kidogo ya mji wa Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# ZBS yapiga 'stop' uingizaji bidhaa za waya za kili

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Viwango Zanzibar (ZBS) imepiga marufuku uingizaji, matumizi na usambazaji wa bidhaa ya waya wa umeme yenye jina la kili cable baada ya kugundulika kuwa chini ya viwango.

Mkurugenzi Mkuu wa ZBS, Yussuph Majid Nassor, alisema wamefikia hatua hiyo baada ya kupewa taarifa za kuwapo kwa bidhaa hiyo sokoni zilizoingizwa nchini na mfanyabiashara asiyefahamika.

Alisema kuwa baada ya kupata taarifa kutoka kwa wasamaria wema, ZBS ilichukua sampuli za bidhaa hiyo na kuifanyia uchunguzi wa kimaabara na kugundulika kutokidhi viwango vilivyowekwa.

"Tulichukua hatua ya kufanya ukaguzi na kuchukua sampuli za waya yenye jina la kili kwa ajili ya kuipima na ripoti ya upimaji wa sampuli hii ikabainika kuwa bidhaa hiyo imeshindwa katika kipengele cha 'sheath' (unene wa waya wa nje)", alieleza Majid.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa waya huo ulitakiwa kuwa na unene wa milimita 1.5 kulingana na matakwa ya kiwango cha ZBS lakini uligundulika kuwa na milimita 1.05 jambo linaloweza kuleta madhara kwa watumiaji.

Hivyo aliwaomba wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa taasisi pindi wanapobaini bidhaa zenye utambulisho huo.

Aidha, alilishukuru Jeshi la Polisi na Tume ya Ushindani Halali wa Biashara kwa kushiriki operesheni ya kuondoa bidhaa hizo madukani.

Katika hatua nyingine Majid alieleza kuwa mbali ya hatua zilizochukuliwa pia wamelifikisha suala hilo polisi na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi (ZAECA) kwa hatua zaidi kufuatia kunakiliwa kwa bidhaa hiyo jambo ambalo ni kosa kisheria.

"Kwa mujibu wa Sheria ya Viwango Namba 1 ya Mwaka 2011 pamoja na mambo mengine ZBS imepewa jukumu la kulinda ubora wa bidhaa zinazoingizwa au kuzalishwa nchini ili kulinda viwanda na wazalishaji halali, ndiyo maana suala hili tumelifikisha huko ili kulinda haki za AfriCab", alisema.

Alisema ZBS inaendelea na uchunguzi juu ya bidhaa hizo na taarifa za kuwapo kwa mchele uliorudishwa baada ya kukosa viwango katika masoko ya Zanzibar na kwamba hatua zitachukuliwa kwa wahusika.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, bidhaa hizo zimegunduliwa kuwapo sokoni Mei 11, mwaka huu, taasisi hiyo kufanya operesheni ya kuziondoa baada ya kuzifanyia uchunguzi na kubaini kuwa hazikukaguliwa kabla wala baada ya kuingia nchini kupitia mifumo ya taasisi hiyo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**DOTTO MANYASI LAZARO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba: **S.4430/0055/2015** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **LUSHAMBA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2015. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **LIN/LW/RB/168401/2023**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**BRUNO GASPER NGOWI** Anatangaza kupotelewa na cheti cha Kidato cha nne chenye index namba **S. 0357-0071** kilichotolewa na Baraza la mitihani kupitia shule ya Sekondari ya Uru Secondary School mwaka 2017

Yeyote atakaye kiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa polisi: KIL/MOS/RB/12840/2023**

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE**
**NO. 12/2023**
**In the Matter of the Estate of the Late**
**KASHIMENT STANLEY MAGUNILA**
**And**
**In the Matter of the Application for Later of Administration by**
**STANLEY YUSUPH MAGUNILA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 of 1963)**

**ALL PERSON c**laiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grand of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be field on or before the 16 day of June, 2023.

**Dated at Korogwe this 17 day of May, 2023.**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**VERONICA RAYMOND MINJA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number S.2376-0150 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MUGABE SEKONDARI mwaka 2015. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KW/RB/82/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI NA GARI

**JOHN VICENT JOSEPH** anatangaza kupotea kwa kadi za pikipiki zenye namba za usajili **MC 355 CVC, MC 256 CNB, MC 894 CJZ, MC 997 CJR, MC 422 CJF, MC 110 CFK, MC 383 BFU, MC 102 BFR, MC 218 BCR, MC 515 AVJ, MC 801 ABS, MC 196 AJB, MC 179 AJB, MC 181 AJB, MC 190 AJB, MC 948 ASK** na kadi ya gari yenye namba za usajili T 769 BLH. Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya polisi: **ARU/MUR/RB/165998/2023.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI

**RAMADHANI ISSA SHABANI** anatangaza kupotea kwa kadi ya bajaji aina ya **BOXER** yenye usajili namba: **MC365 DBD**, chassis namba: **MD2B15BX2MWE94911.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DAR/OST/RB/124259/2023**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**LILILOKO DODOMA**
**MAOMBI MADOGO NA.145 YA MWAKA 2023**
**ALICE MSANGAA..................MDAI**
**VERSUS**
**JOHN SANGA............ MDAIWA**
**KWA:**
**JOHN SANGA**
**POPOTE ULIPO.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayomaelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili Wewe binafsi,Wakili au Mwakilishi yoyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 22.06.2023 saa 3.00 asubuhi. Kwa mujibuwa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.

**ANGALIZO:** Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu,Baraza likithibitisha kuwa umepokea Hati ya Wito,Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe **15 ya Mwezi wa MEI,2023**

.................................................

**MWENYEKITI**
**Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,**
**DODOMA**

**FOMU MIRATHI - 2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MOROGORO**
**Kituo cha MJINI Mkoa MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na. 43 /2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU RASHIDI MOHAMED TUNDUGURU WA MAFINGA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA AMINA RASHIDI TUNDUGURU**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe **26 Mwezi 05 Mwaka 2023.** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

Endapo kama yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

* Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa

* Marehemu hakuacha wosia * Futa isiyohusika

Imetolewa leo tarehe **17 Mwezi wa 05 Mwaka 2023.**

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

## KUPOTELEWA NA KADI ZA GARI

Ndugu **PAUL AMANIELI CHIKIRA** anatangaza kupotelewa na kadi za gari aina ya **(TOYOTA LANDCRUISER, ISUZU, TOYOTA- TRUENO)** zenye namba za usajili **T 452 AUM, T 715 ARA, T 653 AQK**. Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **MOR/MOR/RB/155094/2023**

Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu naye.

*OFISI ZA MATANGAZO*
*Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.*
*Mobile:*
*+255 - 745 700 710.*
*E-mail:*
*advertise@guardian.co.tz,*
*Website:*
*www.ippmedia.com*

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa

Tupigie 0677020701

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

MAKALA MAALUM

# Mlipuko wa UVIKO-19 ulivyowatikisa wafanyabishara wa soko nyumbani

## • Wapo walioanguka, hawakunyanyuka tena

**Na Gwamaka Alipipi**




Shughuli za kibiashara katika Soko la Kimataifa Kariakoo, kunakodaiwa kuathirika sana katika zama za mlipuko wa corona. **PICHA: MTANDAO.**

MLIPUKO wa ugonjwa virusi vya corona, licha ya athari zake kiafya, pia kuna wafanyabiashara waliokuwa na mitaji mikubwa, sasa wameanguka. Wako katika lindi la umasikini.

Uchunguzi wa Nipashe mkoani Dar es Salaam, umebaini tangu kuwapo mlipuko wa ugonjwa mwaka 2019, kuna baadhi ya wafanyabiashara waliokuwa na kipato kikubwa, wameathirika hata kufikia umasikini.

Pia, imebainika baadhi ya wafanyabiashara waliomiliki maduka mawili hadi matatu, sasa wanamiliki moja, wengine wakibadili aina ya biashara hadi kwenye ujasiriamali.

**WAELEZA KILICHOWASIBU**

Isaak Barnabas, aliyekuwa mfanyabiashara mkubwa wa nguo za watoto, Mtaa wa Congo, Kariakoo, Dar es Salaam, ambako biashara zake zimekuwa katika mgomo, anasema umempa hasara ambayo hatoisahau.

"Mambo yalivurugika, tulikuwa hatujui tushike lipi tuache lipi, kila kitu kilikuwa 'shaghalabaghala'. Wateja hawakuwapo wala bidhaa hazinunuliki," anasema Isaak.

Anataja hasara aliyopata ni Sh. milioni 14, baada ya mzigo aliyoagiza China kukwama kufika Tanzania, hata nguo alizokuwa nazo dukani nazo hazikuuzika.

"Niliagiza balo 10, kila moja likiwa thamani ya Sh. milioni 1.4, ghafla nikasikia katika taarifa ya habari kwamba kuna ugonjwa umeingia China unaitwa corona na umesababisha meli na ndege zisitoke nchini humo. Kwa kweli niliishiwa nguvu, nikikumbuka ninalia sana, hadi leo sijapata mizigo yangu," anasema.

Anafafanua alitegemea mzigo akiuza alipe kodi ya pango la biashara Sh. milioni tisa kwa muda wa miezi sita, hivyo akakwama na kuamua kufunga biasharaa. Akarudi nyumbani.

Rahabu Mbinga, mfanyabishara wa duka la jumla la vitenge sokoni Kariakoo, anaieleza Nipashe kwamba mwaka 2019 wakati wa mlipuko wa ugonjwa corona, biashara yake ilikwama.

Anasimulia akashindwa kuuza bidhaa zake, kutokana na wateja kuogopa kufika Kariakoo kwa hofu ya kuambukizwa ugonjwa huo. Akakaa na mzigo muda mrefu pasipo kuuzwa.

Mbinga anasema kuwa kabla ya mlipuko wa ugonjwa huo, mauzo ya siku yalikuwa Sh. milioni tano, lakini yalishuka hadi Sh. 400,000.

Mwingine, Philipo Mallya, muuzaji wa vifaa vya simu za mkononi eneo la Mwenge, Dar es Salaam, anasimulia alivyoagiza maboksi 15 ya vifaa vya simu kutoka China. lakini zilikwama na hakuzifuata.

"Niliweka mtaji wangu wote huko, niliagiza mzigo wa Sh. milioni 20, kwa sababu awali niliagiza mzigo wa Sh. milioni saba nikapata faida ya Sh. milioni 13, hivyo nikaagiza mzigo mkubwa zaidi lakini nilichoambulia, Mungu ndiye anajua, kwa sasa niko tu nyumbani," anasema.

Baadhi ya wafanyabiashara, kinamama na wasichana kwenye maeneo kadhaa ya Dar es Salaam, wanaieleza Nipashe waliyoyaona wakati wa mlipuko wa virusi vya corona.

Zainabu Almasi (58), anayeishi Wazo Hill, muuzaji wa vyakula Tegeta Sokoni, anaielezea corona ilikuja bila taarifa, yeye na wenzake hawakuwa wamejiandaa.

Anafafanua kuwa ilisababisha kula mtaji wake wa kununua vyakula kama vile mchele, unga, sukari, mafuta ya kupika na viungo.

Mama Lishe, Khadija Ulanga, anakiri corona ilimshinikiza aishiwe fedha, kwa sababu wateja wake wengi walipotea.

Tutindaga Mwakipesile (38) anayeishi Boko, muuzaji wa vyakula na mpambaji sherehe, anasema biashara yake iliporomoka katika kipindi cha janga la corona.

"Nilikuwa na wasichana tisa ninafanya nao hizo kazi. Ilibidi kuwaachisha kazi, kwa sababu tulikuwa hatupati tenda tena, kwa kuwa shughuli hizo zilisitishwa rasmi na serikali kuzuia mikusanyiko ya watu," anasema.

**SERIKALI YAELEZA**

Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, anakiri corona imeletea athari kubwa katika sekta zake, akirejea mwaka 2022, thamani ya mauzo ya bidhaa kwenda Soko la Ulaya ilipungua hadi Dola za Marekani milioni 955.6, kutoka Dola za Marekani milioni 1,346.1 za mwaka 2021. Ni sawa na upungufu asilimia 29.1.

**CHAMA WAFANYABIASHARA**

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wakulima (TCCIA), Nebart Mwapwele, anasema biashara nyingi ziliathirika kwa mlipuko wa ugonjwa huo.

Anasema ni hali ikasababisha biashara ndogo na kubwa kudorora, kampuni zilipunguza wafanyakazi kujinusuru na hali mbaya ya kiuchumi.

Mwapwele anasema nchi nyingi zilifunga mipaka iliyosababisha wafanyabiashara nchini washindwe kwenda kuuza bidhaa na kushindwa kupata wateja.

Viwanda vya ujenzi vilisimamisha uzalishaji kutokana na kukosa malighafi ya uendeshaji walizokuwa wanaagiza kutoka nje.

**JUMUIYA WAFANYABIASHARA**

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania (JWT), Hamis Libembe, anasema mlipuko wa ugonjwa corona uliwaacha asilimia 20 ya wafanyabiashara masikini.

Anasema wafanyabiashara walioagiza bidhaa kutoka nje, waliathirika, kwa sababu viwanda vingi vilifungwa na nchi kuweka masharti magumu kwa wageni kuingia.

"Baadhi ya nchi waliweka utaratibu kwa mgeni lazima ukae karantini siku 14 hadi 21, ndipo uingie nchini mwao, kutokana na usumbufu wafanyabiashara wengi wa Tanzania waliacha kusafiri," anasema.

Libembe anaendelea: "Wafanyabiashara 295 wakubwa na wadogo walilazimika kusitisha kufanya shughuli zao kutokana na hasara waliyoipata kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya corona."

Anafafanua kuwa idadi kubwa ya wafanyabiashara walifunga biashara zao, kwa sababu waliogopa kusafiri kwenda kuchukua bidhaa nje ya nchi, hata walipoagiza hawakupata mizigo yao.

**HATUA ZA BENKI KUU**

Kamati ya Sera na Fedha ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) iliyokutana Mei, 2020 ikapitisha hatua za kisera kukabiliana na athari za mlipuko wa ugonjwa corona kiuchumi.

Eneop moja linatajwa ni kushusha kiwango cha chini cha kisheria cha sehemu ya amana zinazowekwa na benki kinachotakiwa kuwekwa BoT, kutoka asilimia saba hadi sita .

Pili, BoT ilishusha kiwango cha riba inayotozwa kwa benki kukopa kutoka asilimia saba hadi tano, kuanzia Mei 12, 2020. Hiyo inaelezwa kwa BoT ikaongeza wigo wa benki kukopa kwa riba nafuu, kupunga riba ya mikopo kwa wateja.

Tatu, BoT ikaongeza unafuu kwenye dhamana na hati fungani za kiserikali zinazotumika na benki kama dhamana ya kukopa kutoka BoT.

Hatua nyingine ya BoT, ikajadiliana na wakopaji namna ya kurejesha mikopo na kutoa unafuu wa urejeshaji wa mikopo inavyoonekana inafaa.

Tano, kampuni zinazotoa huduma za kifedha kwa njia ya mtandao kuongeza kiwango cha miamala kwa siku kwa mteja kutoka Sh. milioni tatu hadi milioni tano na kiwango cha akiba kwa siku kwa mteja kutoka Sh. milioni tano hadi Sh. milioni 10.

Sita, BoT ikaendelea kufanya tathmini ya athari za ugonjwa corona katika sekta mbalimbali za uchumi na kuchukua hatua stahiki kupunguza madhara yake.

**WASOMI WASHAURI**

Wataalamu wa uchumi na biashara wametoa maoni yao, namna serikali inakabili majanga ya pindi dhahama aina hiyo.

Mchumi Benjamin Mwamsojo anashauri serikali kuiboresha sekta ya kilimo, ili taifa liwe na malighafi ya kutosha kulisha viwanda na kuacha kutegemea zaidi nje.

Anasema serikali ijiwekeze katika kuboresha thamani ya shilingi, sambamba na sekta ya fedha kwa ujumla.

Mtaalamu wa Fedha na Uchumi, Dk. Steven Mloza, anasema wafanyabiashara wanapaswa kuwekeza katika mauzo ya moja kwa moja.

Anasema takwimu za Shirika la Fedha Duniani (IMF) zinaonyesha uchumi wa dunia ulipungua kwa asilimia 4.4 mwaka 2020, wakati mauzo ya moja kwa moja yalikua kwa takribani asilimia 2.3.

Dk. Mloza anataja mauzo ya moja kwa moja ndio yaliongeza biashara na nafasi za ajira kwa asilimia kubwa, kuliko maeneo mengine katika kipindi cha maafa ya UVIKO-19.

# MWAMUZI APIGWA, MECHI YAVUNJIKA LIGI KUU Z'BAR

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MCHEZO wa Ligi Kuu Zanzibar kati ya KMKM na Black Sailor ulivunjika dakika ya 83 baada ya mwamuzi wa mechi hiyo, Ibrahimu Ali Ubwa, kupata kichapo kutoka kwa wachezaji wa Black Sailor.

KMKM iko katika mbio za kuwania ubingwa wa ligi hiyo wakati Black Sailor yenyewe inapambana kujinusuru na janga la kushuka daraja.

Mechi hiyo iliyochezwa juzi jioni ilishindwa kumalizika baada ya KMKM kufunga bao la kusawazisha.

Mchezo huo ulichezwa kwenye Uwanja wa Mau A, juzi na ulikuwa wa mzunguko wa 28 wa Ligi Kuu Zanzibar ambayo ipo ukingoni.

Ubwa alilazimika kuvunja mechi hiyo baada ya kutokea kadhia hiyo iliyomfanya kushindwa kuendelea na majukumu yake huku timu hizo zikiwa sare ya bao 1-1.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Zanzibar, Hashim Salum, alisema bodi yake inasubiri kupokea ripoti ya mwamuzi na kamishna wa mchezo huo kwa ajili ya kuifanyia kazi.

Salum alisema bodi hiyo itatoa uamuzi haraka ili kuepuka kuathiri matokeo ya michezo mingine pamoja na msimamo wa ligi hiyo hasa katika mbio za ubingwa na pia kufahamu timu moja iliyobakia itakayoungana na nyingine tatu ambazo zimeshashuka daraja.

Alisema awali bodi hiyo ilitoa tahadhari kwa timu kuelekea lala salama kuhakikisha wanaonyesha nidhamu na kudhibiti hasira zao hasa wanapopata matokeo wasiyoyatarajia.

"Vitendo vya fujo ya aina yoyote vitakavyopelekea kuharibu mchezo havikubaliki katika soka, tutahakikisha tunawachukulia adhabu kali wote watakaopatikana na hatia kwa mujibu wa kanuni za mashindano," alisema Salum.

Hata hivyo bosi huyo amewataka viongozi wa timu zinazoshiriki Ligi Kuu Zanzibar kuzungumza na wachezaji wao kabla ya mchezo na kuwakumbusha kutoingia majukumu ya waamuzi hasa pale wanapoona hawajaridhika.



Wachezaji wa mpira wa kikapu wa timu ya JMK Park wakifanya mazoezi ili kujiimarisha katika viwanja vya Jakaya Youth Kikwete Park, Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# MeridianBet yaongeza mkwanja

**Na Saada Akida**

KAMPUNI ya mchezo wa kubashiri Meridianbet Tanzania kupitia kasino ya mtandaoni imekuja kivingine kwa shabiki anayecheza sloti ya Wild Hot 40 kwa kushinda mkwanja mrefu zaidi.

Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano Meridianbet Tanzania, Martin Nkurlu, alisema jana mchezo wa kasino wa matunda unapendwa na wachezaji wengi kwa sababu mchezaji matumaini ya kuongeza fedha kwenye dau analiloweka na kufanya kuwa Jackpot tatu za ushindi ambazo ni Gold, Platinum na Diamond.

"Sloti hii ya Wild Hot 40 inapatikana Meridianbet kasino ya mtandaoni, inasifika kwa uchezaji wake rahisi haswa katika mtandaoni, inasifika kwa uchezaji wake rahisi hasa katika muundo wa alama za matunda na muundo wa kolamu tano na mistari 40 ya malipo," alisema Nkurlu.

Aliongeza matunda hayo ni ndizi, tufaa (Apple) na Strawberry ambapo ukipata alama tano, utapata mara 2.5 ya dau uliloweka ukipata alama tano za kengele, unarudishiwa mara tano ya dau ulililoweka.

"Ukipata alama saba za bahati, utapata mara 10 ya dau ulililoweka, ukipata alama tano za Wild, utarudishiwa mara 25 ya dau ulililoweka wakati ukipatia alama tano za Scatter unarudishiwa zaidi ya mara 500 ya dau lako," aliongeza.

Alisema pia ukisajili Meridianbet unapewa bonasi ya mizunguko 50 bure kucheza michezo ya kasino ya mtandaoni.

## Kapombe, Zimbwe vinara wa 'assist'

**Na Adam Fungamwango**

MABEKI wa Simba, Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr' na Shomari Kapombe, wanaongoza kwa kutoa pasi za mwisho zilizozaa mabao upande wa mabeki mpaka sasa ambapo zimebaki raundi mbili ili kukamilika kwa msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara, imeelezwa.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Bodi ya Ligi ya Tanzania, Kapombe na Zimbwe Jr, wote wameshatoa 'assist' sita mpaka sasa ambapo kama itakwenda hivi hadi mwisho wataweka rekodi ya kuwa mabeki waliongoza kutoa pasi za mwisho katika Ligi Kuu Bara msimu huu wa 2022/23.

Wakati Kapombe akiwa ni beki wa kulia na kutegemewa wa Simba, Zimbwe ni beki wa kushoto na kutumainiwa na timu hiyo iliyoondolewa katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika hivi karibuni.

Nafasi ya pili kwa mujibu wa takwimu hizo inashikiliwa na Nicholaus Gyan wa Singida Big Stars ambaye ana 'assist' tano mpaka sasa, Joyce Lomalisa wa Yanga akikamata nafasi ya tatu na 'assist' zake nne, Amos Kadikilo wa Geita Gold na Djuma Shaaban wa Yanga hawa wana 'assist' mbili kila mmoja.

Takwimu zingine zilizotolewa ni makipa waliocheza mechi nyingi bila kuruhusu lango kuguswa, ambapo kipa wa Yanga, Djigui Diarra amekuwa kinara kutokana na kuwa na 'clean sheets' 16 mpaka sasa. Hakuna kipa yoyote anayemfikia, hivyo tayari ameshakuwa mshindi kwa msimu huu.

Aishi Manula wa Simba anafuatia kwa kuwa na 'clean sheets' 12, Ali Ahmada wa Azam FC akiwa nazo nane, Metacha Mnata, ambaye amezichezea Singida Big Stars na Yanga ana 'clean sheets' saba, huku makipa Benjamin Haule, Mahmoud Mroivil wa Coastal Union, Fikirini Bakari wa Ihefu na Said Kipao wa Kagera Sugar wenye 'clean sheets' sita kila mmoja.

Straika wa Yanga, Fiston Mayele akiwa na mabao 16 mpaka sasa anawaongoza kwa kupachika magoli huku kiungo mshambuliaji wa Simba, Clatous Chama, yeye anaongoza kwa 'assist' za jumla, akiwa ameshatoa pasi za mwisho 14 mpaka sasa, kiungo mwingine, Saido Ntibazonkiza, ambaye aliichezea Geita Gold na baadaye Simba, yeye amechangia mabao 22, ambayo ni mengi kwenye ligi kuliko mchezaji mwingine yoyote, akiwa amefunga mabao 10 na 'asist' 12.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### KANE ATAKIWA PSG

MSHAURI wa soka wa Paris St-Germain, Luis Campos, amekutana na wawakilishi wa mshambuliaji wa Tottenham Hotspur, Harry Kane, mwenye umri wa miaka 29 kuhusu uwezekano wa mabingwa hao wa Ufaransa kumsajili nahodha huyo wa England. ***(Foot Mercato)***

### MBAPPE, BELLINGHAM HAO

REAL Madrid inataka kumsajili mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wamiaka 24 kutoka PSG na mlinzi wa kushoto wa Bayern Munich, Alphonso Davies (22), pamoja na kiungo wa kati wa Borussia Dortmund na England, Jude Bellingham (19), msimu huu. ***(Sky Sports)***

### SLOT ATAKIWA SOKONI

KLABU ya Feyenoord inatarajia kumpa mkataba mpya kocha raia wa Uholanzi, Arne Slot, mwenye umri wa miaka 44 ili kuzuia nia ya Tottenham Hotspur. ***(Mail)***

### MESSI, NEYMAR WATAKIWA

BARCELONA inataka kumsajili tena mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Argentina, Lionel Messi, mwenye umri wa miaka 35 na mshambuliaji wa Brazil, Neymar (31), kutoka PSG. ***(Football Transfers)***

### ARSENAL, BARCA VITANI

ARSENAL na Barcelona zinavutiwa na kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Ilkay Gundogan, mwenye umri wa miaka 32, ambaye anataka mkataba wa zaidi ya mwaka mmoja kubakia Manchester City. ***(SportBild)***

### BAYERN KUMUUZA MANE

BAYERN Munich iko tayari kumuuza mshambuliaji wa Senegal, Sadio Mane mwenye umri wa miaka 31 katika msimu wa joto na hawana uwezekano wa kutumia chaguo la kubadilisha uhamisho wa mkopo wa mlinzi wa Ureno, Joao Cancelo kutoka Manchester City hadi uhamisho wa kudumu kwa pauni milioni 60 utakapomalizika. ***(Mirror)***

### XHAKA KUTUA LEVERKUSEN

BAYER Leverkusen ipo katika mazungumzo ya kina na Arsenal kuhusu kumsajili kiungo wa kati wa Uswizi, Granit Xhaka, mwenye umri wa miaka 30 kwa dau la takribani pauni milioni 13. ***(Standard)***

### ABRAHAM ATAJWA CHELSEA

MSHAMBULIAJI wa AS Roma, Tammy Abraham, amesema mlinzi wa Chelsea na England, Reece James, mwenye umri wa miaka 23 amemwambia arejee Stamford Bridge, huku Manchester United na Newcastle United pia zikimtaka mchezaji huyo. ***(Tuttomercatoweb, via Standard)***

### DAHOUD ATAKIWA BRIGHTON

KLABU ya Brighton inatarajiwa kumsajili kiungo wa kati wa Ujerumani, Mahmoud Dahoud, mwenye umri wa miaka 27 ambaye mkataba wake unamalizika kule Borussia Dortmund msimu wa joto. ***(Football Insider)***

### MILNER KUREJEA LEEDS

LEEDS United italazimika kupambana kubakia Ligi Kuu England ili kupata nafasi ya kumrejesha kiungo wa kati, James Milner (37), katika klabu hiyo, Ingawa bado wanapewa nafasi kubwa ya kumpata mchezaji huyo wakati mkataba wake utakapokamilika msimu huu wa joto. ***(Mail)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# OFA MPYA KUINUNUA UNITED YAWASILISHWA

●●●Ni kutoka kwa Shekhe Jassim na inaelezwa ni ya mwisho ambayo...

**MANCHESTER, England**

SHEKHE Jassim amewasilisha ofa ya mwisho iliyoboreshwa zaidi katika jaribio lake la kuinunua Manchester United kutoka kwa familia ya Glazer, Shirika la Habari la PA, limesema.

Sheikh Jassim, Mwenyekiti wa Benki ya Kiislamu ya Qatar na mtoto wa waziri mkuu wa zamani wa nchi hiyo, na mpinzani wake Sir, Jim Ratcliffe walikuwa wamewasilisha ofa zao zilizotarajiwa kuwa za tatu na za mwisho kwa klabu hiyo mwezi uliopita.

Lakini huku kukiwa na imani na kambi ya Ratcliffe, Sheikh Jassim ameongeza thamani ya ofa yake, ambayo kama hapo awali ni ya asilimia 100, kwani italipa madeni yote na inajumuisha mfuko tofauti unaoelekezwa kwa klabu na jumuiya zake. Viongozi na wafanyakazi ndani ya Old Trafford wana hamu ya kupata ufafanuzi juu ya hali ya mauzo ambayo ilianza Novemba, mwaka jana wakati United ilitangaza bodi ilikuwa ikitafuta "njia mbadala" za kuimarisha ukuaji wa klabu, huku chaguo moja la mauzo likizingatiwa.

Sheikh Jassim alikuwa mmiliki mtarajiwa wa kwanza kuthibitisha hadharani wakati ofa yake ya ilipowasilishwa kwa mara ya kwanza Februari na hivi karibuni alijiunga na Ratcliffe, Mmiliki wa INEOS mzaliwa wa Manchester.

Robo ya kwanza ya mwaka ilitambuliwa hapo awali kama wakati muhimu katika mchakato ambao umevuma na kutishia kuficha shinikizo la United la kufuzu kushiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Tarehe ya mwisho ya Februari ilifuatiwa na tarehe ya mwisho ya Machi kwa wale walioendelea, na Raine Group, iliyoletwa kusimamia uuzaji, kisha kuuliza wahusika kwa zabuni yao ya tatu na ya mwisho mnamo Aprili 28, mwaka huu.

Mashabiki wa United wameweka wazi nia yao ya kutaka kuuzwa kikamilifu kwa klabu hiyo ili itoke miknoni mwa familia ya Glazers, ambao hawakuwa maarufu tangu walipoinyakua klabu hiyo mwaka 2005.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,114,9

MECHI KALI

SEVILLA FC
VERSUS
JUVENTUS

1 | 2.39
X | 3.13
2 | 2.92

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money

SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# INZAGHI: INTER HATUIHOFII MAN CITY AU REAL MADRID



**MILAN, Italia**

KOCHA wa Inter Milan, Simone Inzaghi, amekiri timu yake haitakuwa tishio kubwa katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Manchester City au Real Madrid baada ya kukamilisha ushindi mnono wa mabao 3-0 dhidi ya AC Milan kwenye mechi ya nusu fainali iliyochezwa juzi.

Bao la Lautaro Martinez dakika ya 74 kwenye Uwanja wa San Siro liliifanya Inter kuwashinda wapinzani wao wa jiji moja kufuatia ushindi wa magoli 2-0 katika mechi ya kwanza ya wiki iliyopita.

Alipoulizwa kama angependelea katika mchezo wa fainali kumenyana na City au Madrid, ambao jana walitarajiwa kucheza mchezo wa mkondo wa pili wa hatua ya nusu fainali, Inzaghi alisema anamtarajia yoyote.

"Ni kawaida unapoenda kukutana na City au Real unaonekana ni mdogo, lakini soka huwa wazi: tulikutana na Real Madrid mwaka jana na tukapoteza mechi mbili, lakini tulicheza vizuri, tutaangalia na yeyote atakayefika."

City na Madrid zimetoka sare ya bao 1-1 baada ya mechi yao ya kwanza nchini Hispania wiki iliyopita.

"Yoyote tutakayemalizana naye, itakuwa sawa tu kwa sababu ni timu mbili kubwa zenye ubora wa ajabu," alisema Inzaghi.

"Nitatazama mechi yao, kama nilivyotazama mkondo wa kwanza ... Ni wazi tutaifuatilia kwa karibu."

# Xhaka ateta na Leverkusen

**LONDON, England**

KLABU ya Bayer Leverkusen iko katika mazungumzo ya kumsajili kiungo wa Arsenal, Granit Xhaka, vyanzo vimeambia ESPN.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 amebakiza mwaka mmoja katika mkataba wake wa sasa na ingawa Washika Bunduki hao wana chaguo la kuongeza mwaka mmoja zaidi, vyanzo vinasema klabu hiyo bado haijakifikiria kipengele hicho.

Hilo limezua sintofahamu akilini mwa kiungo huyo juu ya mustakabali wake na Leverkusen imetafuta kufaidika kwa kuwafuata Arsenal na kuwapa ofa inayoaminika kuwa ya euro milioni 15.

Mkataba bado haujakamilika, lakini Xhaka yuko tayari kuondoka ikiwa Arsenal hawako tayari kumpa mkataba mpya wa muda mrefu zaidi.

Arsenal inataka kurekebisha safu yao ya kiungo msimu huu wa joto na imemlenga Declan Rice wa West Ham, ingawa mchezaji huyo wa kimataifa wa England huenda akagharimu pauni milioni 100 au zaidi.



## HABARI MICHEZO


65,687/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 20/05/23 | 17:00 | Fulham FC vs Crystal Palace | 2.33 | 3.30 | 2.80 |
| 02. 20/05/23 | 17:00 | Wolverhampton Wanderers vs Everton FC | 2.55 | 3.25 | 2.55 |
| 03. 20/05/23 | 17:30 | FC Arouca vs GD Chaves | 2.44 | 3.25 | 2.70 |
| 04. 20/05/23 | 18:00 | FC Nantes vs Montpellier HSC | 2.12 | 3.40 | 3.10 |
| 05. 20/05/23 | 19:15 | KVC Westerlo vs Standard Liege | 2.27 | 3.20 | 2.60 |
| 06. 20/05/23 | 22:00 | Lille OSC vs Olympique Marseille | 2.25 | 3.45 | 2.80 |
| 07. 21/05/23 | 00:30 | Botafogo FR RJ vs Fluminense FC RJ | 2.65 | 3.30 | 2.44 |
| 08. 21/05/23 | 00:30 | America FC MG vs Fortaleza EC CE | 2.45 | 3.40 | 2.60 |
| 09. 21/05/23 | 14:30 | Club Brugge vs Royal Antwerp FC | 2.23 | 3.20 | 2.65 |
| 10. 21/05/23 | 15:30 | SK Rapid Wien vs LASK | 2.33 | 3.20 | 2.50 |
| 11. 21/05/23 | 15:30 | West Ham United vs Leeds United | 2.22 | 3.35 | 2.95 |
| 12. 21/05/23 | 16:30 | FSV Mainz vs VfB Stuttgart | 2.35 | 3.40 | 2.70 |
| 13. 21/05/23 | 19:00 | SSC Napoli vs Inter Milano | 2.90 | 3.25 | 2.28 |
| 14. 21/05/23 | 19:00 | Adana Demirspor vs Besiktas Istanbul | 2.48 | 3.30 | 2.29 |
| 15. 21/05/23 | 19:30 | KRC Genk vs Union Saint-Gilloise | 2.17 | 3.20 | 2.75 |
| 16. 21/05/23 | 21:30 | CA Belgrano vs CA Talleres de Cordoba | 2.95 | 2.85 | 2.22 |
| 17. 21/05/23 | 22:30 | Sporting Lisbon vs Benfica Lisbon | 2.48 | 3.45 | 2.50 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 18/05/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2512 | Motala Aif vs Bodens BK | 1.97 | 3.59 | 3.08 |
| 14:00 | 2116 | Torslanda IK vs IK Zenith | 1.50 | 4.77 | 4.45 |
| 14:00 | 3937 | Viby IF vs VRI | 1.39 | 4.67 | 6.02 |
| 14:00 | 4925 | SV Sonsbeck vs FSV Duisburg | 1.22 | 5.60 | 7.00 |
| 15:00 | 1298 | Piteaa IF vs FC Stockholm Internazionale | 3.34 | 3.70 | 1.85 |
| 15:00 | 3714 | US Lecce youth vs Sassuolo Youth | 2.19 | 3.11 | 3.11 |
| 15:00 | 3888 | Hvidovre IF vs Sonderjyske | 2.01 | 3.35 | 3.19 |
| 15:00 | 4602 | IK Gauthiod vs Stenungsunds IF | 2.46 | 3.73 | 2.35 |
| 16:00 | 1440 | SV Neuhof vs Baunatal | 3.38 | 3.89 | 1.83 |
| 16:00 | 1530 | Bor. Freialdenhoven vs FC Hurth | 2.06 | 3.92 | 2.79 |
| 16:00 | 2098 | Pdrm vs Negeri Sembilan | 4.21 | 3.49 | 1.71 |
| 16:00 | 2195 | Wegberg-Beeck vs FC Pesch | 1.32 | 4.99 | 7.06 |
| 16:00 | 2590 | 1.fc Monheim vs Ssvg Velbert | 5.40 | 4.50 | 1.37 |
| 16:00 | 3171 | Yxhults IK vs IFK Skovde FK | 2.70 | 3.68 | 2.19 |
| 16:00 | 3387 | Mjallby vs BK Hacken | 4.09 | 3.52 | 1.75 |
| 16:00 | 5095 | Kray vs Uerdingen | 7.85 | 5.79 | 1.25 |
| 16:30 | 3211 | Fortuna Koln II vs Spvg Frechen 20 | 2.53 | 3.73 | 2.29 |
| 16:30 | 5699 | Turu Dusseldorf 1880 vs VfB Homberg | 4.15 | 4.15 | 1.62 |
| 17:00 | 2071 | IK Oddevold vs Oskarshamns Aik | 1.50 | 3.84 | 5.53 |
| 17:00 | 2389 | Herrestads AIF vs Grebbestads IF | 2.26 | 3.68 | 2.59 |
| 17:00 | 3109 | Sollentuna Utd FF vs Umeaa FC | 2.20 | 3.48 | 2.71 |
| 17:00 | 3362 | Eskilsminne IF vs Aatvidaberg | 1.89 | 3.35 | 3.56 |
| 17:00 | 3546 | SK Super Nova vs Jelgava | 3.32 | 3.58 | 1.92 |
| 17:00 | 3564 | Valur vs UMF Grindavik | 1.07 | 9.74 | 16.58 |
| 17:00 | 5005 | Wiener Neustadt vs ASV Drassburg | 2.74 | 3.57 | 2.19 |
| 17:00 | 5460 | Stjarnan vs Keflavik IF | 1.74 | 3.90 | 3.74 |
| 17:30 | 1131 | Peykan FC vs MES Rafsanjan | 4.10 | 3.11 | 1.87 |
| 17:30 | 2786 | Foolad Khuzestan vs Aluminium Arak | 2.59 | 2.70 | 2.91 |
| 17:30 | 2985 | Naft Masjed Soleyman FC vs Malavan Bandar Anzali | 4.09 | 3.11 | 1.87 |
| 17:30 | 3869 | Esteghlal Tehran vs Teraktor Sazi | 1.91 | 3.20 | 3.77 |
| 17:30 | 3899 | Zob Ahan vs Havadar | 2.23 | 2.85 | 3.32 |
| 17:30 | 5062 | Gol Gohar vs Sanat Naft Abadan | 2.50 | 2.86 | 2.86 |
| 17:45 | 4788 | Wolfsburg W vs SC Freiburg W | 1.16 | 7.05 | 10.36 |
| 18:00 | 1049 | Copenhagen vs Aalborg | 1.62 | 3.57 | 4.97 |
| 18:00 | 1341 | Sparta Prague B vs Dukla Prague | 2.26 | 3.24 | 2.78 |
| 19:00 | 1945 | Al Shabab Riyadh vs Al Wehda | 1.34 | 5.01 | 7.90 |
| 19:00 | 2990 | Narpes Kraft vs FC Vaajakoski | 2.05 | 3.52 | 3.05 |
| 19:00 | 3360 | Abha vs Al-Ettifaq | 2.26 | 3.35 | 3.03 |
| 19:00 | 5591 | Throttur Reykjavik vs Breidablik | 14.48 | 9.10 | 1.09 |
| 20:00 | 2727 | Zamalek vs Aswan | 1.97 | 3.21 | 3.76 |
| 20:00 | 4568 | Fenerbahce vs Trabzonspor | 1.57 | 4.10 | 4.94 |
| 20:00 | 5274 | HK Kopavogs vs KA Akureyri | 3.06 | 3.43 | 2.08 |
| 21:30 | 1363 | Usd Audace Cerignola vs Foggia | 2.31 | 2.98 | 2.93 |
| 21:30 | 4683 | Newcastle vs Brighton | 1.96 | 3.66 | 3.26 |
| 22:00 | 2140 | Sevilla FC vs Juventus | 2.39 | 3.13 | 2.92 |
| 22:00 | 2807 | AZ Alkmaar vs West Ham | 2.52 | 3.32 | 2.62 |
| 22:00 | 4508 | Sheffield Wed vs Peterborough | 1.67 | 3.84 | 4.55 |
| 22:00 | 5414 | FC Basel vs Fiorentina | 4.15 | 3.84 | 1.73 |
| 22:00 | 5492 | Bayer Leverkusen vs Roma | 2.03 | 3.23 | 3.59 |
| 22:45 | 3817 | Fylkir vs KR Reykjavik | 2.06 | 3.30 | 2.85 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# AZAM FC MACHO YOTE UBINGWA KOMBE LA FA

**Na Saada Akida**



BAADA ya kutinga hatua ya fainali ya mashindano ya Kombe la FA, uongozi wa Azam FC umesema wamejipanga vizuri kuhakikisha wanashinda mechi hiyo na kumaliza msimu huu wakiwa wameshinda taji hilo.

Azam FC itacheza fainali ya Kombe la FA kwa kukutana na mshindi kati ya Yanga na Singida Big Stars ambao wanakutana Jumapili kwenye Uwanja wa CCM Liti ulioko Singida.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2013/14 wamesonga mbele katika mashindano hayo kwa kuifunga Simba mabao 2-1

Matajiri hao wa Chamazi walipotea mapema katika mbio ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na kutolewa pia kwenye michuano ya kimataifa hatua za awali.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat' (pichani), alisema wanaimani na kikosi chao itafanya vizuri katika mchezo huo wa fainali na wako tayari kukutana na timu yoyote kati ya Singida Big Stars au Yanga.

Popat alisema baada ya kutofikia malengo ya kutwaa taji la ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambalo limechukuliwa na Yanga, matumaini yao yameeleka katika kulinyakua Kombe la FA.

"Tumejipanga vizuri na tayari tumeongeza nguvu kwenye benchi la ufundi kwa kumleta, Youssouph Dabo, ambaye ndiye kocha wetu kwa sasa, tuna matumaini makubwa kutoka kwake, pia wachezaji wanahitaji fainali hiyo," alisema Popat.

Yanga ndio mabingwa watetezi wa mashindano hayo ambayo bingwa wake anakwenda katika michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

# Pamba yaipania Mashujaa FC

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Pamba FC, Yusuph Chipo, amesema kikosi chake kiko tayari kwa mechi ya mtoano dhidi ya Mashujaa FC itakayochezwa Mei 21, mwaka huu kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma.

Pamba inacheza mechi hiyo baada ya kumaliza katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi ya Championship sawa na Mashujaa iliyomaliza kwenye nafasi hiyo katika First League.

Chipo aliliambia gazeti hili wamejipanga kufanya vyema katika mechi hiyo na bado hawajakata tamaa ya kupanda kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

"Tunaendelea na mazoezi hapa kwenye uwanja wetu wa Nyamagana, tunataka kwenda kuivaa Mashujaa tukiwa imara, tutaenda kupambana, hatujakata tamaa, hadi kieleweke," alisema kocha huyo.

Tayari JKT Tanzania ya Dar es Salaam na Kitayosce kutoka Tabora zimeshapanda daraja kucheza Ligi Kuu Bara msimu ujao huku Ruvu Shooting ya Mlandizi, Pwani ikiwa imeshateremka.

Wakati huo huo, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima, juzi alikabidhi Sh. milioni tatu kwa Pamba FC baada ya timu hiyo kupata ushindi wa mabao 2-1 katika mechi yake ya mwisho ya Ligi ya Championship dhidi ya Transit Camp.

Michezo

Alhamisi Mei 18, 2023

Nipashe



UKURASA 21

## Ofa mpya kuinunua United yawasilishwa

# YANGA SC YAWEKA REKODI

### ●●●Ni baada ya kutinga kibabe fainali Kombe la Shirikisho CAF na...



Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele (kulia), akijiandaa kumtoka beki wa Marumo Gallants, Gumede katika mechi ya hatua ya nusu fainali iliyochezwa kwenye Uwanja wa Royal Bafokeng, Rustenburg nchini Afrika Kusini jana. Yanga ilishinda mabao 2-1. **PICHA: MTANDAO**

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE Yanga imeweka historia. Ikiwa na miaka 88 tangu kuanzishwa kwake mwaka 1935, imetinga hatua ya fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika baada ya kuifunga wenyeji Marumo Gallants mabao 2-1 katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Royal Bafokeng, Afrika Kusini.

Yanga imesonga mbele kwa jumla ya mabao 4-1, baada ya mechi ya mkondo wa kwanza iliyofanyika Mei 10, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kushinda mabao 2-0.

Walikuwa ni wachezaji wawili wa kimataifa kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Fiston Mayele na Mzambia, Kennedy Musonda waliopachika mabao hayo ambayo mbali na kuwapeleka fainali, yakavunja rekodi ya timu hiyo ya Sauzi kutopoteza mechi nyumbani kwao.

Yanga, inakuwa ni timu ya pili ya Tanzania kufanya hivyo, baada ya Simba kuingia fainali kama hizo mwaka 1993, wakati huo ikiitwa Kombe la CAF, kabla ya kubadilishwa na kuitwa Kombe la Shirikisho mwaka 2004.

Ilitinga hatua hiyo kwa kuifunga, Atletico Sport Aviacao ya Angola mabao 3-1 nchini, kabla ya kwenda kutoa suluhu ugenini.

Hata hivyo Mabingwa hao wapya wa Tanzania Bara, wana nafasi kubwa ya kuivunja rekodi hiyo kwa kutwaa kombe hilo ambalo Simba ilishindwa kufanya hiyo ilipofungwa mabao 2-0 mbele ya Rais Mstaafu, Ali Hassan Mwinyi, dhidi ya Stella Abidjan ya Ivory Coast kwa mabao yaliyofungwa dakika ya 17 na Desre Kouome na lile la dakika ya 77 lililofungwa na Jean Bolizozo.

Katika mechi ya nusu fainali ya jana, sekunde chache kabla ya mapumziko, Mayele aliipeleka mbele Yanga kwa kupachika bao akiwazidi mbio mabeki wa Marumo Gallants na kupiga shuti lililopanguliwa na kipa Washington Arubi, lakini haukwenda mbali na ukampoteza pia maboya, mpigaji akauwahi na kuusindikiza wavuni.

Bao lililowanyong'onyesha Wasauzi hao na mashabiki wake wachache waliojitokeza kwenye mechi hiyo na kumezwa na wageni, liliwekwa ndani ya kimia na Musonda dakika ya 61.

Ilifanana kwa kiasi kikubwa na bao la kwanza, Mayele aliondoka na mpira katika ya uwanja, akijua udhaifu mabeki wa wapinzani wake kwenye mbio, alipiga mbele na kuanza kushindana nao kasi, akawazidi, akiwa pembeni upande wa kulia mwa uwanja, aliingia ndani kidogo na kupiga krosi ilimkuta Musonda, aliyeukwamishwa wavuni na mguu wa kushoto.

Kabla ya mechi ya marudiano, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, alibainisha wapinzani wake ni wazuri kwenye eneo la ushambuliaji, lakini hawako vizuri katika idara ya ulinzi hasa kujibu mashambulizi.

Shambulio la kwanza kwenye mechi hilo lilifanyika dakika ya 10, kwa staili ile ile ya 'counter attack', alipoondoka na mpira kwa umbali mrefu, akampa Kennedy Musonda ambaye alimrudishia, lakini kwa bahati nzuri kipa, Arubi alikuwa ametokea na kuuwahi.

Dakika ya 25, Ranga Chivaviro, alipata nafasi baada ya kuzuka vurumai kwenye lango la Yanga, lakini akapiga mpira juu ya lango, dakika mbili baadaye, Nku Lebiba naye alikosa bao alipopaisha mpira kama mwenzake.

Kipa wa Yanga, Djigui Diarra, aliokoa bao la wazi akiwa yeye na Celimpilo Ngema, dakika ya 32, ambaye akipiga shuti lililompoteza, lakini mguu wake wa kulia alitumia kuuokoa mpira huo ukazaa kona tasa.

Bao la kufutia machozi wa wenyeji lilifungwa dakika ya 90 na Chivarivo, aliporuka juu na kujitwisha mpira wa kichwa, kwa mpira mrefu uliopigwa na Lucky Mohomi.

Kwa matokeo hayo, Yanga sasa inamsubiri mshindi kati ya USM Alger ya Algeria ambayo jana usiku mkubwa ilikuwa nyumbani Uwanja wa Juillet wa Tano ikiwakaribisha ASEC Mimosas kutoka Ivory Coast.

## Simba 'kupindua' usajili wa mastaa

**Na Saada Akida**

WAKATI Simba ikihitaji kumaliza msimu kwa heshima, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Roberto Oliviera 'Robertinho' amesema atafanya 'mapinduzi makubwa' katika mchakato wa usajili kwa ajili ya kuboresha kikosi kuelekea msimu ujao.

Akizungumza na Nipashe jana, Robertinho alisema wanajua walipokosea na wanafanya tathmini ya kila idara ili warekebishe makosa na kujenga kikosi imara kitakachowapa mafanikio.

Robertinho alisema kwa msimu huu kila mmoja ndani ya Simba ametimiza wajibu wake kwa kiasi kikubwa, kilichotokea ni matokeo ya mpira.

"Ni mapema kusema nani na nani tutasajili lakini nimepanga kufanya mabadiliko makubwa. Nafanya kazi kwa misingi ya taaluma yangu, kama unavyojua soka ni mchezo wa wazi, nitaendelea kuwa na kundi la wachezaji ambao wanajituma na kufanya kazi kwa moyo mmoja," alisema Robertinho.

Aliongeza tayari mapendekezo ya awali ameshayapeleka kwa mabosi wa klabu hiyo na anaimani yatafanyiwa kazi kwa wakati kwa sababu wanataka kuingia msimu mpya wakiwa bora zaidi.

## JKT Queens yatwaa ubingwa wanawake

**Na Mwandishi Wetu**

MAAFANDE wa JKT Queens wametwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania msimu wa 2022/23 baada ya kuichapa Mkwawa Queens mabao 7-2 katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Samora, Iringa jana.

Matokeo hayo yameifanya JKT Queens kuwavua ubingwa Simba Queens baada ya kufikisha pointi 46, huku Wekundu wa Msimbazi ambao jana waliwafunga Ceasiaa Queens bao 1-0 wakifikisha pointi 45.

JKT Queens sasa itapata tiketi ya kuiwakilisha Tanzania katika mashindano ya Afrika Mashariki na Kati yatakayofanyika kuanzia Juni 3 hadi 17, mwaka huu jijini Nairobi, Kenya.

Mechi nyingine za funga pazia la ligi hiyo imeshuhudiwa Fountain Gate Princess wakishinda mabao 6-0 dhidi ya The Tigers huku Yanga Princess iliyokuwa ugenini Lindi ikipata ushindi wa magoli 3-1.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >